ISSN 0856-6976

# TAMKO LA SERA YA FEDHA

*Mapitio ya Nusu Mwaka*
*2024/25*

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Februari 2025**

ISSN 0856-6976

# TAMKO LA SERA YA FEDHA

## *Mapitio ya Nusu Mwaka 2024/25*

**GAVANA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

Februari 2025

6 Februari 2025

**Mhe. Dkt. Mwigulu L. Nchemba (Mb),**
**Waziri wa Fedha,**
**Mji wa Serikali-Mtumba,**
**Barabara ya Hazina,**
**S. L.P 2802,**
**40468 Dodoma.**

Mheshimiwa Waziri,

**BARUA YA WASILISHO**

Kifungu namba 21, cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197, kinaitaka Benki Kuu ya Tanzania kutoa **Tamko la Sera ya Fedha** mwezi Juni kila mwaka, likifuatiwa na tathmini ya nusu mwaka inayotolewa mwezi Februari. Tamko hili linaainisha mwelekeo wa sera ya fedha na utekelezaji wake katika kufikia malengo ya kiuchumi yaliyowekwa na Serikali. Kwa muktadha huo, nawasilisha kwako Mapitio ya Nusu Mwaka ya **Tamko la Sera ya Fedha kwa mwaka 2024/25**, kwa ajili ya kuwasilishwa Bungeni.

Tamko hili la Sera ya Fedha linatoa tathmini ya mwenendo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini pamoja na utekelezaji wa sera ya fedha na matokeo yake katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25. Aidha, Tamko hili linabainisha mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini, pamoja na mwelekeo wa sera ya fedha kwa nusu ya pili ya mwaka 2024/25, katika kufikia malengo yake.

Wasalaam,

Emmanuel M. Tutuba
Gavana
Benki Kuu ya Tanzania

## YALIYOMO


**BARUA YA WASILISHO** .................................................... **i**
**Muhtasari** .................................................... **iv**

**SEHEMU YA KWANZA** .................................................... **1**
UTANGULIZI .................................................... 1

**SEHEMU YA PILI** .................................................... **5**
2.0 MALENGO NA UTEKELEZAJI WA SERA YA FEDHA KATIKA NUSU YA KWANZA YA MWAKA 2024/25 .................................................... 5
2.1 Malengo ya Sera ya Fedha .................................................... 5
2.2 Utekelezaji wa Sera ya Fedha .................................................... 5

**SEHEMU YA TATU** .................................................... **8**
3.0 MWENENDO WA UCHUMI WA DUNIA .................................................... 8
3.1 Ukuaji wa Uchumi wa Dunia .................................................... 8
3.2 Mfumuko wa Bei .................................................... 9
3.3 Mwenendo wa Bei za Bidhaa Katika Soko la Dunia .................................................... 11

**SEHEMU YA NNE** .................................................... **14**
4.0 HALI YA UCHUMI NCHINI .................................................... 14
4.1 Pato la Taifa .................................................... 14
4.2 Mfumuko wa Bei .................................................... 18
4.3 Mwenendo wa Ujazi wa Fedha na Mikopo kwa Sekta Binafsi .................................................... 22
4.4 Viwango vya Riba .................................................... 25
4.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali .................................................... 27
4.6 Deni la Taifa .................................................... 29

4. 7 Mwenendo wa Sekta ya Nje ........................................... 32
4. 8. Ukwasi wa Fedha za Kigeni na Viwango vya Kubadilisha Fedha za Kigeni ........................................... 38
4.9 Mwenendo wa Sekta ya Fedha ........................................... 42
4.10 Mifumo ya Malipo ........................................... 43

**SEHEMU YA TANO ........................................... 47**
5.0 MATARAJIO YA HALI YA UCHUMI ........................................... 47
5.1 Mwelekeo ya Uchumi wa Dunia ........................................... 47
5.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Ndani ........................................... 48

**SEHEMU YA SITA ........................................... 49**
6.0 SERA YA FEDHA KATIKA NUSU YA PILI YA MWAKA 2024/25 ........................................... 49
6.1 Mwelekeo wa Sera ya Fedha ........................................... 49
6.2 Sera ya Riba ........................................... 50
6.3 Sera ya Ubadilishaji Fedha za Kigeni na Akiba ya Fedha za Kigeni ........................................... 51

VIAMBATISHO ........................................... 52

# MUHTASARI

## Malengo na matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha

Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25, Kamati ya Sera ya Fedha ya Bodi ya Benki Kuu ilipanga riba ya Benki Kuu (CBR) kuwa asilimia 6 kwa kila robo ya mwaka. Uamuzi huu ulilenga kuhakikisha utekelezaji wa sera ya fedha unaendelea kudhibiti mfumuko wa bei kutokana na kupungua kwa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni na kuendelea kuchagiza ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Ili kuhakikisha ukwasi unakidhi mahitaji ya shughuli za uchumi nchini, Benki Kuu ilihakikisha riba ya mikopo ya siku saba baina ya benki inakuwa tulivu, ndani ya wigo wa asilimia +/- 2 wa Riba ya Benki Kuu (CBR).

Utelekezaji wa sera ya fedha katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25 ulikuwa wa kuridhisha. Kiwango cha ukwasi kiliendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi, mfumuko wa bei uliendelea kuwa mdogo, chini ya lengo la asilimia 5, na mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa kasi ya kuridhisha na kuchangia ukuaji wa uchumi. Aidha, utekelezaji wa sera ya fedha, pamoja na kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni nchini, ulichangia kuimarika kwa thamani ya shilingi, kuondoa soko la fedha za kigeni lisilo rasmi, kupunguza matumizi ya fedha za kigeni katika kufanya miamala na upangaji wa bei za bidhaa na huduma nchini, na kupunguza vishawishi vya kuhodhi fedha za kigeni kwa matarajio ya kushuka kwa thamani ya shilingi (*exchange rate speculation*).

Riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha baina ya benki ilikuwa tulivu na ndani ya wigo isipokuwa katika miezi ya Agosti, Septemba na Oktoba 2024, ambapo iliongezeka kidogo na kuvuka wigo wa juu wa CBR. Kuongezeka kwa riba hiyo kulitokana na ongezeko la mahitaji ya fedha taslimu kwa ajili ya kununua mazao hususan korosho, tumbaku

na nafaka, kufuatia kiasi kikubwa cha mavuno kuliko matarajio, benki za biashara kuongeza uwekezaji katika rasilimali zilizo katika fedha za kigeni, na ongezeko la uwekezaji wa wananchi katika dhamana za Serikali hivyo kupunguza amana zao katika benki za biashara. Katika kukabiliana na hali hii, Benki Kuu iliongeza ukwasi katika uchumi kwa kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki za biashara (*reverse repurchase agreements),* kununua fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni, na kubadilishana na benki za biashara fedha za kigeni kwa shilingi (*foreign exchange swap*). Vilevile, Benki Kuu iliongeza ukwasi kwa kununua dhahabu kupitia programu yake ya ununuzi wa dhahabu katika soko la ndani. Kufuatia hatua hizi, ukwasi katika benki uliimarika na riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha baina ya benki ilipungua na kurudi ndani ya wigo wa CBR.

**Mwenendo wa uchumi wa dunia**

Uchumi wa dunia uliimarika katika nusu ya pili ya mwaka 2024, kutokana na utelekelezaji wa sera ya fedha na hatua zilizochukuliwa na baadhi ya serikali kwa ajili ya kuchagiza shughuli za kiuchumi, na kuongezeka kwa mahitaji ya walaji. Ripoti iliyochapishwa na Umoja wa Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD) mwezi Desemba 2024 inaonesha kuwa uchumi wa dunia ulikua kwa asilimia 3.2 mwaka 2024, huku ripoti za Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia za mwezi Januari 2024 zikikadiria ukuaji wa kati ya asilimia 3.2 na 2.7, mtawalia.

Mfumuko wa bei ulipungua katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25 ukilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2023/24, ukielekea kufikia malengo ya benki kuu za nchi mbalimbali duniani. Aidha, mfumuko wa bei ulipungua katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), isipokuwa

kwa nchi chache zilishindwa kufikia vigezo vya mtangamano wa kiuchumi, hasa kutokana na changamoto za ukame na kupungua kwa thamani ya sarafu za nchi husika. Bei za bidhaa katika soko la dunia zilikuwa na mwenendo tofauti. Bei ya mafuta ghafi ilipungua kutokana na ongezeko la uzalishaji kutoka nchi zisizo wanachama wa Umoja wa Nchi Zinazozalisha Mafuta Duniani (OPEC), na kupungua kwa mahitaji nchini China. Bei ya dhahabu iliendelea kuwa juu, kutokana na ongezeko la mahitaji ya dhahabu fedha kwa ajili ya uwekezaji.

**Mwenendo wa uchumi wa Tanzania**

Uchumi wa Tanzania bara na Zanzibar uliendelea kuwa imara mwaka 2024. Kwa upande wa Tanzania Bara, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 5.6 katika robo tatu za kwanza za mwaka 2024, na unakadiriwa kukua kwa asilimia 5.7 katika robo ya nne. Kutokana na mwenendo huu, ukuaji wa uchumi wa Tanzania bara kwa mwaka 2024 unatarajiwa kuwa asilimia 5.6, juu kidogo ya maoteo ya awali ya asilimia 5.4. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, huduma za fedha na bima, usafirishaji na ujenzi. Kwa upande wa Zanzibar, uchumi ulikua kwa asilimia 7 katika robo tatu za kwanza za mwaka 2024, na unakadiriwa kufikia asilimia 7.2 kwa mwaka mzima. Ukuaji huu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuimarika kwa shughuli za utalii, ufugaji na ujenzi.

Mfumuko wa bei uliendelea kuwa tulivu katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25. Mfumuko wa bei kwa Tanzania Bara ulikuwa takriban asilimia 3, chini ya lengo la nchi la muda wa kati la asilimia 5, ukiendana na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kwa nchi za EAC na SADC. Utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha na bajeti, utulivu wa bei za chakula, pamoja na kupungua kwa bei za bidhaa za petroli katika soko la dunia kulichangia kwa kiasi kikubwa utulivu wa mfumuko wa bei. Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei pia umeendelea kupungua

na kufikia wastani wa asilimia 5.1, kutokana na kushuka kwa bei ya bidhaa za chakula na zisizo za chakula.

Ukuaji wa ujazi wa fedha na mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuwa wa kuridhisha. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa takriban asilimia 12 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25, ukichangiwa zaidi na ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 16.1, sanjari na utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kuhakikisha utulivu wa bei nchini. Mikopo iliyoelekezwa katika shughuli binafsi, ambayo hujumuisha mikopo kwa biashara ndogondogo na za kati (SMEs), iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote iliyotolewa kwa sekta binafsi na kuendelea kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Riba za mikopo na amana hazikuwa na mabadiliko makubwa ikilinganishwa na viwango vilivyorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Aidha, riba za mikopo zilikuwa takriban asilimia 16, na riba za amana zilikuwa asilimia 8. Riba za mikopo zinatarajiwa kuendelea kupungua kutokana na maboresho yanayoendelea kufanywa na Benki Kuu na Serikali katika kukabiliana na changamoto za kimuundo.

Utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa upande wa Tanzania Bara ulikuwa wa kuridhisha. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25, mapato ya ndani yaliendana na malengo, yakichangiwa na kuimarika kwa shughuli za uchumi pamoja na maboresho katika usimamizi na ukusanyaji wa kodi. Kwa upande wa Zanzibar, utekelezaji wa bajeti ulikuwa wa kiwango cha juu, ambapo mapato ya Serikali yalivuka lengo kwa asilimia 4.8. Mapato ya kodi yalivuka lengo kwa asilimia 3.6, kutokana na maboresho katika usimamizi wa kodi pamoja na utayari wa wananchi kulipa kodi kwa hiari. Kwa serikali zote, matumizi yaliendelea kufanyika kwa kuzingatia upatikanaji wa mapato.

Deni la Serikali limeendelea kuwa himilivu. Katika mwaka unaoishia 2023/24, uwiano wa thamani ya sasa (*Present Value*) ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ulikuwa asilimia 41.1, chini ya ukomo wa uhimilivu wa deni ulioainishwa katika Mwongozo wa Uhimilivu wa Deni kutoka IMF na Benki ya Dunia wa asilimia 55, na kigezo cha mtangamano wa kiuchumi kwa nchi za EAC cha ukomo wa asilimia 50. Aidha, uwiano wa deni la umma  (katika bei za sasa), lilikuwa asilimia 46.3 ya Pato la Taifa, chini ya kigezo cha mtangamano wa kiuchumi kwa nchi za SADC cha ukomo wa asilimia 60.

Sekta ya nje iliendelea kuimarika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25, sanjari na mwenendo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini. Urari wa malipo ya kawaida (*current account balance*) unakadiriwa kuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 785.3, takriban nusu ya nakisi iliyorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Hali hii ilitokana na kuimarika kwa shughuli za utalii, na ongezeko la mauzo ya dhahabu, korosho na tumbaku nje ya nchi. Wakati huohuo, urari wa malipo ya kawaida kwa upande wa Zanzibar ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 321.5, ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 219.2, kutokana na ongezeko la mapato yatokanayo na shughuli za utalii.

Robo ya kwanza ya mwaka 2024/25 ilikabiliwa na changamoto ya kupungua kwa ukwasi wa fedha za kigeni. Hata hivyo, katika robo ya pili, ukwasi wa fedha za kigeni uliongezeka kwa kiasi kikubwa. Ongezeko hili lilitokana na kuimarika kwa mazingira ya kiuchumi duniani hususan kushuka kwa viwango vya riba ya sera ya fedha katika nchi zilizoendelea kiuchumi na kupungua kwa bei za mafuta ghafi. Aidha, mapato ya fedha za kigeni kutokana na shughuli za utalii, mauzo ya dhahabu, korosho, na tumbaku yalichangia kuongezeka kwa ukwasi wa fedha za kigeni. Vilevile, utekelezaji wa sera ya fedha uliofanywa

na Benki Kuu ulisaidia kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni nchini. Thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani ilipungua katika robo ya kwanza ya mwaka 2024/25, kisha kuimarika kwa kiwango kikubwa katika robo ya pili. Akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa ya kutosha, ikiongezeka hadi dola za Marekani milioni 5,546.1, mwishoni mwa Desemba 2024. Kiasi hiki kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa muda wa miezi 4.5.

Kufuatia utulivu wa uchumi, sekta ya fedha iliendelea kuwa thabiti, ikiwa na viwango vya chini vya vihatarishi. Sekta ya benki iliendelea kuwa na ukwasi na mtaji wa kutosha, na kutengeneza faida. Rasilimali za benki ziliongezeka sambamba na amana zikichochewa na ongezeko la huduma za uwakala wa benki, pamoja ongezeko la matumizi ya mifumo ya kidijitali katika utoaji wa huduma za kibenki. Ukwasi katika benki uliendelea kuwa wa kutosha na mikopo chechefu ilipungua hadi kufikia asilimia 3.3 mwishoni mwa mwezi Desemba 2024 kutoka asilimia 4.1 mwishoni mwa mwezi Juni 2024. Mifumo ya malipo iliendelea kufanya kazi kwa ufanisi huku Benki Kuu ya Tanzania ikiendelea kuboresha mifumo kwa lengo la kuongeza ufanisi na upatikanaji wake. Aidha, Benki Kuu iliendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuongeza matumizi ya kidijitali katika kufanya miamala nchini badala ya kutumia fedha taslimu.

**Matarajio ya uchumi wa dunia**

Ripoti za uchumi zilizotolewa hivi karibuni na OECD, IMF na Benki ya Dunia zinakadiria ukuaji wa uchumi wa dunia kufikia kati ya asilimia 2.7 na 3.3 mwaka 2025. Matarajio haya yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa sera za fedha na hatua zinazochukuliwa na serikali mbalimbali katika kuchochea shughuli za kiuchumi, na ongezeko la matumizi ya walaji. Hata hivyo, ukuaji huu unaweza

kuathiriwa na kutotabirika kwa sera za kiuchumi, migogoro ya kisiasa, na athari za mabadiliko ya tabia nchi. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kupungua katika nchi nyingi, kutokana na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia na matokeo ya utekelezaji wa sera za fedha iliyopunguza ukwasi katika kipindi kilichopita. Shirika la IMF linakadiria mfumuko wa bei kufikia asilimia 4.2 mwaka 2025, kabla ya kupungua zaidi hadi asilimia 3.5 mwaka unaofuata. Nchi zilizoendelea zinatarajiwa kufikia malengo yao mapema ukilinganisha nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi. Hata hivyo, matarajio kuhusu mfumuko wa bei yanaweza kuathiriwa na migogoro ya kisiasa, athari za mabadiliko ya tabianchi, na ongezeko la bei za nishati.

**Matarajio ya uchumi wa hapa nchini**

Uchumi wa Tanzania Bara unatarajiwa kuendelea kukua kwa kasi ambapo Pato la Taifa (GDP) linatarajiwa kukua kwa takriban asilimia 6 katika nusu ya pili ya mwaka 2024/25. Ukuaji huu utachangiwa zaidi na shughuli za kilimo, ujenzi na huduma za usafirishaji, pamoja na utekelezaji wa sera madhubuti ya fedha na ya bajeti. Kwa upande wa Zanzibar uchumi unatarajiwa kukua kwa zaidi ya asilimia 6, ukichangiwa na shughuli za utalii, ujenzi na upangaji wa majengo. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kuwa tulivu, katika nusu ya pili ya mwaka 2024/25, ukikadiriwa kuwa takriban asilimia 3 kwa Tanzania Bara na chini ya asilimia 5 kwa Zanzibar. Mwenendo huu utachangiwa na utekelezaji wa sera madhubuti ya fedha na ya bajeti, uwepo wa chakula cha kutosha nchini, utulivu wa thamani ya Shilingi na bei za bidhaa katika soko la dunia. Hata hivyo, mfumuko wa bei unaweza kuongezeka endapo nchi za OPEC+ zitaamua kuendelea kupunguza kiwango cha uzalishaji wa mafuta.

**Mwelekeo wa sera ya fedha kwa mwaka 2024/25**

Katika nusu ya pili ya mwaka 2024/25, mwelekeo wa sera ya fedha utakuwa kama ilivyokuwa katika nusu ya kwanza, huku lengo la sera ya fedha likiwa ni kuhakikisha mfumuko wa bei mdogo wa takribani asilimia 3, na kuchagiza ukuaji wa uchumi ili kufikia angalau asilimia 6. Benki Kuu itaendelea kutumia nyenzo zake za sera ya fedha ili kuhakikisha uwepo wa ukwasi unaoendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi na kuhakikisha riba ya mikopo ya siku saba baina ya benki inabaki ndani ya wigo wa riba ya Benki Kuu. Katika kuongeza ufanisi wa sera ya fedha, Benki Kuu itaendelea kufanya maboresho mbalimbali katika soko la fedha baina ya mabenki. Maboresho haya ni pamoja na kufanya mapitio ya dhamana zinazotumiwa na benki za biashara wakati wa kukopa toka Benki Kuu, na viwango vya riba ya mikopo ya siku moja (*lombard loans*) na nyenzo nyingine zinazotumika katika utekelezaji wa sera ya fedha. Vilevile, Benki Kuu itaendelelea kutoa elimu kwa wadau na umma kwa ujumla kuhusu mfumo wa utekelezaji wa sera ya fedha unaotumia riba, na umuhimu wa kutumia Shilingi katika kufanya miamala ya bidhaa na huduma hapa nchini.

**Sera ya riba na viwango vya ubadilishaji fedha za kigeni**

Viwango vya riba vitaendelea kuamuliwa na nguvu za soko. Kamati ya sera ya fedha itaendelea kupanga Riba ya Benki Kuu, ambayo itatoa mwongozo kwa riba zinazopangwa kwenye soko la fedha baina ya benki. Aidha, Benki Kuu itaendelea kufanya maboresho katika sekta ya fedha sambamba na jitihada za Serikali katika kuhakikisha riba za mikopo haziwaumizi wakopaji nchini. Katika kutekeleza haya, Benki Kuu itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya fedha ili kumlinda mtumiaji wa huduma za fedha, kutoa elimu ya fedha na kuongeza huduma jumuishi za fedha. Viwango vya ubadilishaji fedha za kigeni pia vitaendelea kuamuliwa kwa nguvu za soko, hivyo

kusaidia kupunguza madhara yatokanayo na mitikisiko ya uchumi toka nje ya nchi na kuongeza ufanisi wa soko la fedha za kigeni. Benki Kuu itaendelea kushiriki katika soko la jumla la fedha za kigeni (IFEM) kwa mujibu wa Sera ya Ushiriki ya Soko la Fedha za Kigeni (*Foreign Exchange Intervention Policy 2023*). Vilevile, Benki Kuu itaendelea kuhakikisha uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, kama kinga dhidi ya mitikisiko ya kiuchumi kutoka nje ya nchi, na kuhakikisha ushiriki wa benki za biashara katika soko la fedha za kigeni unazingatia miongozo iliyopo.

# SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Tamko la Sera ya fedha kwa mwaka 2024/25 lililotolewa na Benki Kuu ya Tanzania mwezi Juni 2024 liliainisha malengo ya sera za kiuchumi kwa mwaka 2024/25. Malengo haya yaliwekwa kwa kuzingatia Mipango ya Maendeleo ya Taifa na mwenendo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini. Malengo haya yalikuwa ni; (i) kufikia ukuaji wa uchumi wa asilimia 5.4 kwa mwaka 2024 na asilimia 6 kwa mwaka 2025 kwa Tanzania Bara na ukuaji wa asilimia 7.2 na 6.8, kwa Zanzibar, mtawalia[1] na (ii) kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo la asilimia 5 mwaka 2024/25 kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Mapitio haya ya nusu mwaka ya Tamko la Sera ya Fedha la mwaka 2024/25 yanatathmini mwenendo wa uchumi wa dunia na hapa nchini pamoja na matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25. Aidha, Tamko hili linatoa mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini, na sera ya fedha katika nusu ya pili ya mwaka 2024/25.

Pamoja na Sehemu hii ya Utangulizi, Tamko hili limepangwa kwa mtiririko ufuatao: Sehemu ya pili inaainisha malengo na matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25. Sehemu ya tatu inachambua mwenendo wa uchumi wa dunia, ikifuatiwa na Sehemu ya nne inayotathmini mwenendo wa uchumi wa hapa nchini. Sehemu ya tano inatoa mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini. Sehemu ya sita inahitimisha kwa kutoa mwelekeo wa sera ya fedha pamoja na sera za riba na viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni zitakazotekelezwa na Benki Kuu ya Tanzania katika nusu ya pili ya mwaka 2024/25 katika kudhibiti mfumuko wa bei na kuchochea ukuaji wa uchumi.

---

1 Makadirio ya ukuaji wa uchumi kwa Tanzania bara kwa mwaka 2025 yameboreshwa kutoka asilimia 5.8 ya awali.

**Mfumo wa Sera ya Fedha wa Benki Kuu ya Tanzania**

Mfumo wa sera ya fedha ya Benki Kuu ya Tanzania hulenga kudhibiti mfumuko wa bei nchini na kuwezesha ukuaji endelevu wa uchumi. Mnamo mwezi Januari 2024, Benki kuu ilianza rasmi kutekeleza sera ya fedha kwa kutumia mfumo wa riba ili kuongeza ufanisi, sawia na mabadiliko ya mazingira ya kiuchumi. Mfumo huu ambao unazingatia zaidi mwelekeo na matarajio ya mwenendo wa viashiria mbalimbali vya kiuchumi (*forward looking*) hutumia Riba ya Benki Kuu ili kuchagiza mwenendo wa riba za muda mfupi katika masoko ya fedha, ambazo hutarajiwa kuashiria viwango vya riba vya muda mrefu na hatimaye kuathiri mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi. Mambo muhimu katika mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu yameainishwa kama ifuatavyo.

**Lengo la Sera ya Fedha**

Lengo la msingi la sera ya fedha ni kuhakikisha utulivu wa bei, yaani kiwango kidogo na thabiti cha mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei hupimwa kwa kuangalia mabadiliko ya kila mwaka katika fahirisi za bei za walaji nchini ambalo huwasilishwa kwa asilimia. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuwa asilimia 5 katika muda wa kati. Lengo hili ni muafaka kwa ajili ya kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi nchini, pamoja na kuhakikisha utulivu wa riba na thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu za nchi nyingine.

**Lengo la Kati**

Benki Kuu inadhibiti mfumuko wa bei na kuwezesha ukuaji wa uchumi kwa kupanga kiwango cha riba ya Benki Kuu (CBR). Riba hii hupangwa kuendana na maoteo ya mfumuko wa bei, sambamba na ukuaji endelevu wa uchumi.

**Kiashiria cha Utendaji**

Chini ya mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba, Benki Kuu inahakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku 7 katika soko la fedha baina ya benki (lengo la uendeshaji) inaendana na riba ya Benki Kuu ili kufikia malengo ya mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi. Riba ya siku 7 katika soko la fedha baina ya benki imechaguliwa na Benki Kuu kwa kuwa ni tulivu na ina uhusiano wa karibu na riba ya Benki Kuu.

**Nyenzo za Sera ya Fedha**

Benki Kuu ya Tanzania inatumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha ili kuhakikisha kuwa lengo la uendeshaji linaendana na riba ya Benki Kuu. Nyenzo kuu za utekelezaji wa Sera ya fedha ni pamoja na mikopo ya muda mfupi baina ya Benki Kuu na benki za biashara (*repurchase agreement and reverse repurchase agreement*). Nyenzo nyingine ni uuzaji na ununuzi wa dhamana (*debt securities*), na uuzaji na ununuzi wa fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni baina ya benki. Nyenzo nyingine zinazotumika ni pamoja na kiwango cha amana za benki za biashara kinachotakiwa kuwekwa kisheria Benki Kuu (*Statutory Minimum Reserve*) na riba inayotumika kutoza benki au Serikali zinapochukua mikopo Benki Kuu. Pamoja na nyenzo hizo, Benki Kuu pia inatoa mikopo ya muda mfupi ambayo hutakiwa kurudishwa ndani ya siku husika na ile ya siku moja (*Intraday and Lombard loan facilities*) ili kusaidia uwepo wa ufanisi katika mifumo ya malipo na ufanyaji wa miamala. Aidha, Benki Kuu inaweza kutumia nyenzo nyingine za sera ya fedha kuendana na mahitaji ili kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya kisera.

**Uwasilishaji wa Sera ya Fedha kwa Umma**

Benki Kuu ya Tanzania inatekeleza jukumu lake la uandaaji na utekelezaji wa sera ya fedha kwa uwazi. Maamuzi ya Kamati ya Sera ya Fedha,

ikiwemo kuhusu riba ya Benki Kuu huwasilishwa kwenye mkutano wa Gavana na wakuu wa taasisi za kibenki na pia kwa umma kupitia vyombo vya habari. Vilevile, Benki Kuu huandaa na kuchapisha Tamko la Kamati ya Sera ya Fedha na taarifa mbalimbali zinazoainisha mwelekeo wa sera ya fedha, matokeo ya utekelezaji wake na mwenendo wa uchumi kwa ujumla. Taarifa hizo zinapatikana kwenye tovuti ya Benki Kuu.

## Utekelezaji wa Sera ya Fedha

- Mwanzo wa kila mwaka wa fedha, Benki Kuu ya Tanzania hutoa mwelekeo wa sera ya fedha katika Tamko lake la Sera ya Fedha kuendana na malengo ya sera za kiuchumi za Serikali.
- Tamko la Sera ya Fedha huidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu ya Tanzania na kuwasilishwa bungeni kupitia kwa Waziri anayesimamia masuala ya fedha, kama ilivyobainishwa katika kifungu namba 21(5) cha Sheria ya Benki Kuu.
- Utaratibu huo pia unafuatwa wakati ya uandaaji wa Mapitio ya nusu mwaka ya Tamko la Sera ya Fedha, ambayo huainisha maendeleo ya utekelezaji wa sera ya fedha dhidi ya malengo yake, matarajio kwa kipindi cha mwaka kilichosalia, na hatua zitakazochukuliwa ili kufikia malengo ya sera.
- Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ya Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu, ambayo inaongozwa na Gavana, inawajibika kuamua kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) kila robo mwaka, kuendana na malengo ya sera za kiuchumi za Serikali.
- Kamati ya Ufuatiliaji na Uangalizi ya Menejimenti ya Benki Kuu inakutana kila siku kutathmini mwenendo wa riba ya mikopo ya siku 7 baina ya mabenki (kiashiria cha uendeshaji) na kuamua hatua zitakazochukuliwa ili kuhakikisha riba hiyo inabaki ndani ya wigo unaotakiwa.

# SEHEMU YA PILI

## 2.0 MALENGO NA UTEKELEZAJI WA SERA YA FEDHA KATIKA NUSU YA KWANZA YA MWAKA 2024/25

### 2.1 Malengo ya Sera ya Fedha

Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25, Kamati ya Sera ya Fedha ilipanga Riba ya Benki Kuu (CBR) katika kiwango cha asilimia sita (6) kwa lengo la kudhibiti mfumuko wa bei unaotokana na kupungua kwa thamani ya Shilingi na kuendelea kuchagiza shughuli za kiuchumi. Maamuzi haya yalizingatia mwenendo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini pamoja na vihatarishi vyake. Katika kuhakikisha uwepo wa kiwango cha ukwasi kinachoendana na mahitaji ya shughuli mbalimbali za kiuchumi, utekelezaji wa sera ya fedha ulilenga kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku saba baina ya benki inabakia ndani ya wigo wa asilimia +/- 2 wa Riba ya Benki Kuu.

### 2.2 Utekelezaji wa Sera ya Fedha


Utelekezaji wa sera ya fedha katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25 ulikuwa wa kuridhisha ambapo kiwango cha ukwasi kiliendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi. Kufuatia utekelezaji huu matarajio ya mfumuko wa bei yaliendelea kuwa chini ya lengo la asilimia 5, huku mikopo kwa sekta binafsi ikiendelea kukua kwa kasi, na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi. Vilevile, utekelezaji wa sera ya fedha pamoja na ongezeko la mapato ya fedha za kigeni nchini, yalichangia kuimarika kwa thamani ya Shilingi na kupelekea kutoweka kwa soko la fedha za kigeni lisilo rasmi, kupungua kwa matumizi ya fedha za kigeni katika kupanga bei na kulipia bidhaa na huduma nchini na kupunguza vishawishi vya kuhodhi fedha za kigeni kwa matarajio ya kushuka kwa thamani ya Shilingi (*exchange rate speculation*).

Riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha baina ya benki ilikuwa tulivu na ndani ya wigo, isipokuwa katika miezi ya Agosti, Septemba na Oktoba, ambapo iliongezeka na kuvuka wigo wa CBR. Kuongezeka kwa riba katika kipindi hicho kulitokana na ongezeko la mahitaji ya fedha kwa ajili ya kununua mazao husussan korosho, tumbaku na nafaka, kufuatia kiasi kikubwa cha mavuno kuliko matarajio, benki za biashara kuongeza uwekezaji katika rasilimali zilizo katika fedha za kigeni, na ongezeko la uwekezaji wa wananchi katika dhamana za Serikali hivyo kupunguza amana zao katika benki za biashara. Katika kukabiliana na hali hiyo ili kuirudisha riba ya mikopo ya siku saba baina ya benki ndani ya wigo wa CBR, Benki Kuu ilitumia nyenzo za sera ya fedha kuongeza ukwasi kwa kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki za biashara (*reverse repurchase agreements),* kununua fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni na kufanya ubadilishanaji wa fedha za kigeni kwa shilingi na benki za biashara (*foreign exchange swap*). Vilevile, Benki Kuu iliongeza ukwasi kupitia Programu ya Ununuzi wa Dhahabu Katika Soko la Ndani[2]. Kufuatia hatua hizi, riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha baina ya benki ilipungua na kuwa ndani ya wigo wa CBR, huku amana za benki katika Benki Kuu (*clearing balances*) zikiongezeka (Kielelezo 2.1a na 2.1b). Vilevile, kupitia utekelezaji wa sera ya fedha, Benki Kuu iliweza kufikia malengo yaliyoainishwa katika *Programu ya Extended Credit Facility (ECF)*, chini ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa Septemba na Desemba 2024[3].

2 Benki Kuu ilianzisha Programu ya Ununuzi wa Dhahabu katika soko la ndani mnamo Septemba 2023, kama moja ya nyenzo za kuongeza akiba ya fedha za kigeni


3 Extended Credit Facility (ECF) ni programu ya IMF yenye lengo la kutoa msaada wa kifedha ndani ya kipindi cha kati kwa nchi wanachama. Programu hii inalenga kusaidia nchi wanachama kufanya maboresho mbalimbali ili kuongeza uthabiti wa uchumi

## Kielelezo 2.1a: Riba ya Benki Kuu na Riba ya Mikopo ya Siku 7




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 2.1b: Amana Za Mabenki na Riba za Mikopo Baina ya Mabenki




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

# SEHEMU YA TATU

## 3.0 MWENENDO WA UCHUMI WA DUNIA

### 3.1 Ukuaji wa Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia uliendelea kuimarika mwaka 2024 kama ilivyo kadiriwa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Benki ya Dunia na OECD. Ukuaji wa uchumi duniani unakadiriwa kuwa asilimia 3.2 mwaka 2024 na unatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 3.3 kwa mwaka 2025 na 2026. Kasi ya ukuaji ilitofautiana baina ya kanda ambapo nchi zilizoendelea zinakadiriwa kukua kwa asilimia 1.9, zinazoibukia na zinazoendela kiuchumi asilimia 4.2, na nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara zikikua kwa asilimia 3.8 (Jedwali 3.1). Kuimarika kwa uchumi wa dunia kunaweka mazingira wezeshi kwa shughuli za uchumi kushamiri hapa nchini.

**Jedwali 3.1: Ukuaji wa Pato la Taifa**

*Asilimia*

| | Halisi | | | Makadirio | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | IMF | OECD | Benki ya Dunia | IMF | OECD | Benki ya Dunia | IMF | Benki ya Dunia |
| | 2024 | | | 2025 | | | 2026 | |
| Dunia | 3.2 | 3.2 | 2.7 | 3.3 | 3.3 | 2.7 | 3.3 | 2.7 |
| Nchi zilizoendelea | 1.7 | n.a | 1.7 | 1.9 | n.a | 1.7 | 1.8 | 1.8 |
| Marekani | 2.8 | 2.8 | 2.8 | 2.7 | 2.4 | 2.3 | 2.1 | 2.0 |
| Eneo la Ulaya | 0.8 | 0.8 | 0.7 | 1.0 | 1.3 | 1.0 | 1.4 | 1.2 |
| Uingereza | 0.9 | 0.9 | n.a | 1.6 | 1.7 | n.a | 1.5 | n.a |
| Japani | -0.2 | -0.3 | 0.0 | 1.1 | 1.5 | 1.2 | 0.8 | 0.9 |
| Nchi zinazoibukia na kuendelea kiuchumi | 4.2 | n.a | 4.1 | 4.2 | n.a | 4.1 | 4.3 | 4.0 |
| Brazili | 3.7 | 3.2 | 3.2 | 2.2 | 2.3 | 2.2 | 2.2 | 2.3 |
| Urusi | 3.8 | n.a | 3.4 | 1.4 | n.a | 1.6 | 1.2 | 1.1 |
| India | 6.5 | 6.8 | 6.5 | 6.5 | 6.9 | 6.7 | 6.5 | 6.7 |
| China | 4.8 | 4.9 | 4.9 | 4.6 | 4.7 | 4.5 | 4.5 | 4.0 |
| Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara | 3.8 | n.a | 3.2 | 4.2 | n.a | 4.1 | 4.2 | 4.3 |

*Chanzo*: Ripoti ya IMF ya Mwelekeo wa Uchumi, Januari 2025, Ripoti ya Benki ya Dunia kuhusu matarajio ya uchumi wa dunia, Januari 2025 na Ripoti ya Mwelekeo wa uchumi ya OECD, Desemba 2024. n.a inamaanisha kuwa takwimu haipo kwa muda ambao repoti hii inaandaliwa.


*Ufafanuzi:* IMF inamaanisha Shirika la Fedha la Kimataifa, na OECD inamaanisha Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo

## 3.2 Mfumuko wa bei

Mfumuko wa bei duniani ulipungua katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25 ukilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Mfumuko wa bei ulikaribia malengo ya benki kuu katika nchi nyingi kufuatia utekelezaji wa sera ya fedha uliolenga kupunguza ukwasi kwenye uchumi na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia (Kielelezo 3.1a). Kufuatia mwenendo huu wa mfumuko wa bei, benki kuu katika nchi zilizoendelea na zile zinazoibukia kiuchumi zilipunguza riba za sera ya fedha. Mwenendo huu wa kupungua kwa mfumuko wa bei ulionekana pia katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na nchi za Jumuiya ya Maendeleo kusini mwa afrika (SADC), ambapo nchi chache zilishindwa kufikia vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kutokana na ukame na kushuka kwa thamani ya sarafu zao (Kielelezo 3.1b na 3.1c).

**Kielelezo 3.1a: Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zilizoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi**


*Asilimia*




*Chanzo*: Ofisi za Takwimu za Nchi husika

## Kielelezo 3.1b: Mfumuko wa Bei kwa Nchi za EAC


*Asilimia*




*Chanzo*: Ofisi za Takwimu za Nchi husika

## 3.1c: Mfumuko wa Bei kwa Nchi za SADC

*Asilimia*




*Chanzo*: Ofisi za Takwimu za Nchi husika


## 3.3 Mwenendo wa Bei za Bidhaa Katika Soko la Dunia

Katika nusu ya kwanza ya 2024/25, bei za bidhaa katika soko la dunia zilikuwa na mienendo tofauti. Bei ya mafuta ghafi ilipungua, ambapo wastani wa mwezi ulikuwa kati ya dola za Marekani 72.29-83.26 kwa pipa, kutokana na ongezeko la uzalishaji kutoka nchi zisizo wanachama wa OPEC na kupungua kwa mahitaji kutoka China.[4] Bei ya dhahabu iliendelea kuwa kubwa, ikiuzwa kwa kati ya dola za Marekani 2,326.44-2,690.06 kwa wakia kutokana na ongezeko la mahitaji ya dhahabu

4 Nchi zisizo wanachama wa OPEC ni Argentina, Brazil, Colombia, Guyana, Mexico, Azerbaijan, Kazakhstan, Qatar, Oman, Angola, Misri na Marekani.


kwa ajili ya uwekezaji, hususan katika wakati ambao uchumi wa dunia unakabiliana na migogoro ya kisiasa (Kielelezo 3.2a). Bei za kahawa ziliongezeka kutokana na sintofahamu iliyojitokeza katika ugavi kufuatia nchi za Ulaya kuanza utekelezaji wa sheria mpya inayokataza ununuzi wa kahawa kutoka nchi zilizoharibu misitu baada ya mwaka 2020. Kwa upande mwingine, bei ya sukari ilipungua kutokana na ongezeko la uzalishaji nchini Brazil na Thailand, ambao ni wazalishaji wakubwa duniani. Aidha, bei ya pamba ilishuka kutokana na kupungua kwa mahitaji pamoja na matarajio ya ongezeko la uzalishaji kufuatia hali nzuri ya hewa katika nchi zinazozalisha pamba kwa wingi (Kielelezo 3.2b).

**Kielelezo 3.2a: Bei za Bidhaa katika Soko la Dunia**




*Chanzo*: http://www.worldbank.org/prospects na Bloomberg

## Kielelezo 3.2b: Bei za Bidhaa katika Soko la Dunia




*Chanzo*: [http://www.worldbank.org/prospects](http://www.worldbank.org/prospects) na Bloomberg

SEHEMU YA NNE


# 4.0 HALI YA UCHUMI NCHINI

## 4.1 Pato la Taifa

Uchumi wa Tanzania Bara na Zanzibar ulikua kwa kasi ya kuridhisha mwaka 2024. Uchumi wa Tanzania Bara ulikua kwa asilimia 5.6 katika robo tatu za kwanza za mwaka 2024, na unakadiriwa kukua kwa asilimia 5.7 katika robo ya nne. Hivyo, ukuaji kwa mwaka 2024 unakadiriwa kuwa asilimia 5.6, ukiwa juu kidogo ya maoteo ya awali ya asilimia 5.4. Ukuaji huu ulichangiwa na shughuli mbalimbali hususan kilimo, huduma za fedha na bima, usafirishaji na ujenzi (Kielelezo 4.1a na 4.1 b). Shughuli za utalii ambazo hutoa mchango mkubwa katika maeneo mengi ya uzalishaji pia zilichangia ukuaji huu kupitia shughuli za usafirishaji, chakula na malazi. Aidha, uwepo wa umeme wa uhakika, hali nzuri ya hewa kwa ajili ya kilimo, kuimarika kwa mazingira ya kibiashara pamoja na utekelezaji wa sera madhubuti za kiuchumi, vilichangia ukuaji huu.


Shughuli za kilimo zilichangia kwa kiwango kikubwa ukuaji huu kwa takriban asilimia 15.9. Wakati huohuo, ongezeko kubwa lilionekana katika uzalishaji wa mazao ya biashara hususan korosho na tumbaku pamoja na nafaka. Kutokana na hali hii, mauzo ya korosho kwa msimu wa mwaka 2024 yalikuwa makubwa kuliko kiwango kilichowahi kufikiwa katika misimu ya miaka mitano iliyopita. Aidha, wakulima walinufaika na bei nzuri kutokana na kuanzishwa kwa mfumo wa kidijitali unaotumika kufanya minada ya mazao ulioanzishwa na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX). Vilevile, shughuli za huduma za fedha na bima, umeme na habari na mawasiliano zilikuwa na ukuaji mkubwa kuliko shughuli nyingine (Kielelezo 4.1c).

## Kielelezo 4.1a: Pato la Taifa




*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu


## Kielelezo 4.1b: Mchango wa Baadhi ya Shughuli za Uchumi katika Pato la Taifa




*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kielelezo 4.1c: Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi**

*Asilimia*





*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Kwa upande wa Zanzibar, uchumi uliendelea kuwa imara ambapo katika robo tatu za kwanza za mwaka 2024, uchumi ulikua kwa asilimia 7.0, na unakadiriwa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2024 (Kielelezo 4.2a). Mwenendo huu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuimarika kwa shughuli za utalii, ufugaji na ujenzi (Kielelezo 4.2b).

## Kielelezo 4.2a: Ukuaji Halisi wa Pato la Taifa kwa Zanzibar


Asilimia




*Chanzo:* Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

## Kielelezo 4.2b: Mchango wa Baadhi ya Shughuli za Uchumi katika Pato la Taifa kwa Zanzabar

Asilimia





*Chanzo:* Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

### 4.2 Mfumuko wa Bei


Mfumuko wa bei uliendelea kuwa tulivu katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25. Katika kipindi hiki, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.1, ukipungua kidogo kutoka asilimia 3.2 katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia (Kielelezo 4.3a na 4.3b). Mwenendo huu ulitokana na utulivu wa bei za vyakula ambavyo huchukua takriban asilimia 28.2 ya mzani wa bei za walaji, pamoja na utekelezaji wa sera madhubuti ya fedha na ya bajeti na kupungua kwa bei ya bidhaa katika soko la dunia. Mwenendo wa bei za vyakula uliakisi uwepo wa chakula cha kutosha katika maeneo mengi nchini kutokana na uwepo wa mvua za kutosha pamoja na upatikanaji na matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo kama mbolea na viuatilifu. Hivyo, mfumuko wa bei za vyakula uliendelea kupungua na kufikia wastani wa asilimia 2.8 katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2024 ukilinganishwa na asilimia 4.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Mfumuko wa bei usiohusisha bidhaa za nishati na vyakula visivyochakatwa (*core inflation*) uliongezeka kidogo na kufikia wastani wa asilimia 3.2 kutoka asilimia 2.5, na uliendelea kuwa na mchango mkubwa katika mwenendo wa mfumuko wa bei (Kielelezo 4.3c).

## Kielelezo 4.3a: Mfumuko wa Bei





*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Kielelezo 4.3b: Mfumuko wa Bei na Malengo ya Nchi na Kikanda




*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Kielelezo 4.3c: Mchango katika Mfumuko wa Bei




*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu


## Jedwali 4.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei

*Asilimia*

| Makundi ya msingi | Uzani(%) | Badiliko la mwezi | | | Badiliko la mwaka | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Dec-23 | Nov-24 | Des-24 | Des-23 | Nov-24 | Des-24 |
| Chakula na vinywaji baridi | 28.2 | 0.6 | 0.5 | 1.6 | 2.3 | 3.3 | 4.6 |
| Vinywaji vyenye kilevi na tumbaku | 1.9 | 0.1 | 0.0 | 0.2 | 4.1 | 1.8 | 2.2 |
| Mavazi na viatu | 10.8 | 0.5 | 0.1 | 0.1 | 3.2 | 1.6 | 1.2 |
| Makazi, maji, umeme, gesi na nishati nyinginezo | 15.1 | 1.5 | 0.9 | 0.1 | 4.0 | 4.1 | 2.9 |
| Samani, vifaa vya majumbani na ukarabati wa makazi | 7.9 | 0.2 | 0.2 | 0.1 | 3.6 | 2.1 | 2.1 |
| Afya | 2.5 | 0.0 | 0.7 | 0.4 | 1.3 | 1.8 | 1.9 |
| Usafiri | 14.1 | 0.6 | 1.1 | -0.5 | 3.3 | 3.8 | 3.5 |
| Habari na mawasiliano | 5.4 | 0.2 | 0.1 | 0.8 | 1.3 | 1.2 | 1.0 |
| Burudani, michezo na utamaduni | 1.6 | 0.2 | 0.5 | 0.1 | 3.5 | 2.0 | 2.0 |
| Huduma za elimu | 2.0 | 0.0 | 1.6 | 0.5 | 3.5 | 3.1 | 3.2 |
| Migahawa na huduma za malazi | 6.6 | -0.1 | 1.3 | -0.1 | 4.3 | 2.6 | 2.8 |
| Huduma za bima na fedha | 2.1 | 0.1 | 0.3 | 0.3 | 0.6 | 1.2 | 1.1 |
| Usafi binafsi, hifadhi ya jamii, bidhaa na huduma mchanganyiko | 2.1 | 1.2 | 3.0 | -0.1 | 4.5 | 6.3 | 5.3 |
| Bidhaa zote (Mfumuko wa bei wa jumla) | 100.0 | 0.6 | 0.7 | 0.5 | 3.0 | 3.0 | 3.1 |
| Makundi yaliyochaguliwa | | | | | | | |
| Fahrisi za msingi (core) | 73.9 | 0.6 | 0.7 | 0.5 | 3.1 | 3.3 | 3.3 |
| Vyakula visivyochakatwa | 20.4 | 0.4 | 0.0 | 0.6 | 2.7 | 1.0 | 2.8 |
| Mafuta, maji na bili za maji | 5.7 | 0.9 | 1.7 | 0.4 | 5.1 | 5.7 | 5.3 |

Kwa upande wa Zanzibar mfumuko wa bei ulipungua kufikia wastani wa asilimia 5.1 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24 (Kielelezo 4.4). Mwenendo huu ulichangiwa na kushuka kwa bei ya bidhaa za vyakula na zisizo za vyakula (Jedwali 4.1). Mfumuko wa bei za vyakula ulipungua hadi asilimia 8, kutoka asilimia 11.6 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24. Kupungua kwa mfumuko wa bei za chakula kulichangiwa na  uwepo wa chakula cha kutosha nchini. Vilevile, mfumuko wa bei za bidhaa zisizo za vyakula, ulipungua hadi asilimia 2.8, kutoka wastani wa asilimia 3.1, kutokana na kupungua bei za bidhaa za nishati.

**Kielelezo 4.4: Mfumuko wa Bei kwa Zanzibar**




*Chanzo*: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

## Jedwali 4.2: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei kwa Zanzibar

*Asilimia*


| Makundi ya msingi | Uzani | Badiliko la kila mwezi | | | Badiliko la Kila mwaka | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Des-23 | Nov-24 | Des-24 | Des-23 | Nov-24 | Des-24 |
| Chakula na vinywaji baridi | 41.9 | -0.2 | -1.0 | 1.1 | 8.4 | 6.5 | 7.9 |
| Vinywaji vyenye kilevi na tumbaku | 0.2 | 0.0 | 0.6 | -8.3 | 0.7 | 25.9 | 15.4 |
| Mavazi na viatu | 6.3 | -0.1 | 0.3 | 1.4 | 2.1 | 0.6 | 2.1 |
| Makazi, maji, umeme, gesi na nishati nyinginezo | 25.8 | 0.6 | -2.6 | -1.1 | 2.4 | 4.6 | 2.8 |
| Samani, vifaa vya majumbani na ukarabati wa makazi | 4.8 | 0.6 | 0.6 | 0.3 | 5.4 | 2.0 | 1.7 |
| Afya | 1.3 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 6.2 | -2.4 | -2.4 |
| Usafiri | 9.1 | -1.6 | -0.5 | -0.1 | 6.7 | -0.3 | 1.2 |
| Habari na mawasiliano | 4.2 | 0.5 | 1.6 | 0.7 | 1.2 | 3.3 | 3.5 |
| Burudani, michezo na utamaduni | 1.1 | 1.1 | 0.0 | 2.1 | 3.5 | 3.8 | 4.9 |
| Elimu | 1.6 | 0.0 | 2.2 | 0.0 | 5.1 | 2.8 | 2.8 |
| Migahawa na huduma za malazi | 1.4 | 1.8 | 0.0 | 0.0 | -1.3 | 15.7 | 0.0 |
| Huduma za bima na fedha | 0.5 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Usafi binafsi, hifadhi ya jamii, bidhaa na huduma mchanganyiko | 1.7 | -0.1 | 0.5 | 0.0 | 2.5 | 0.8 | 0.8 |
| Bidhaa zote (Mfumuko wa bei wa jumla) | 100.0 | 0.0 | -1.0 | 0.4 | 5.5 | 4.5 | 4.9 |
| Makundi yaliyochaguliwa | | | | | | | |
| Chakula | 41.9 | -0.2 | -1.1 | 1.2 | 8.8 | 6.6 | 8.1 |
| Bidhaa zisizo za chakula | 58.6 | 0.2 | -1.0 | -0.3 | 3.2 | 3.0 | 2.5 |

*Chanzo*: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

## 4.3 Mwenendo wa Ujazi wa Fedha na Mikopo kwa Sekta Binafsi


Ukuaji wa ujazi wa fedha na mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuwa wa kuridhisha katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 11.9, ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 15.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24, ukichangiwa zaidi na ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi (Kielelezo 4.5a na 4.5b).

## Kielelezo 4.5a: Ukuaji wa Ujazi wa Fedha na Mikopo kwa Sekta Binafsi




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania


## Kielelezo 4.5b: Mchango wa Ukuaji wa M3




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 16.1 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25, japo kasi ya ukuaji ilikuwa ndogo kuliko ukuaji wa asilimia 19.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Mwenendo huu unaakisi matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kuhakikisha kuwa mfumuko wa bei unaendelea kuwa ndani ya lengo. Uwiano wa mikopo ya sekta binafsi kwa Pato la Taifa ambao huashiria ukuaji wa sekta fedha, ulikuwa asilimia 19.1 katika nusu mwaka ya 2024/25, kutoka asilimia 16.5. Mikopo inayoelekezwa kwa shughuli binafsi ambayo hujumuisha mikopo kwa biashara ndogo ndogo na za kati (SMEs) iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote na kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi (Kielelezo 4.6a na Kielelezo 4.6b). Mikopo iliyotolewa kwa shughuli za kilimo iliongezeka kulinganisha na kipindi kama hicho mwaka 2023/24, kutokana na ongezeko la mahitaji kwa ajili ya ununuzi wa mazao[5].


**Chart 4.6a: Mchango wa Shughuli za kiuchumi katika Ukuaji wa Mikopo, kwa Asilimia**




*Chanzo*: Benki Kuu ya Tanzania

5 Mikopo hii pia haihusishi mikopo inayokwenda kwenye shuguli za kilimo inayotolewa kama Mikopo kwenye Shughuli binafsi *(personal loans)*

## Chart 4.6b: Mgawanyo wa Mikopo kwa Shughuli za Kiuchumi, kwa Asilimia





*Chanzo*: Benki Kuu ya Tanzania

### 4.4 Viwango vya Riba

Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25, riba za mikopo na amana hazikuwa na mabadiliko makubwa kulinganishwa na viwango vilivyorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Riba za mikopo zilikuwa wastani wa takriban asilimia 16, wakati riba za mikopo kwa wateja wakubwa (*negotiated lending rates*) zilibakia takriban asilimia 13 (Kielelezo 4.7a). Riba za amana zilikuwa takriban asilimia 8, wakati riba za amana za wateja wakubwa ziliongezeka kidogo hadi kufikia asilimia 10. Riba za dhamana za serikali ziliongezeka, zikiakisi tabia ya wawekezaji kupendelea kuwekeza katika hatifungani za muda mrefu (Kielelezo 4.7b). Riba za mikopo zinatarajiwa kuendelea kupungua kutokana na hatua zinazochukuliwa katika kukabiliana na changamoto za kimuundo katika soko la fedha. Hatua hizi ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa Kanuni za Kumlinda Mteja wa Huduma za Fedha Nchini za mwaka 2019, kuongeza upatikanaji wa taarifa za


wakopaji kupitia utoaji wa vitambulisho vya Taifa na urasmishaji wa makazi, na kuboresha mfumo wa mahakama ili kuharakisha utatuzi wa migogoro inayohusiana na mikopo.

**Kielelezo 4.7a: Riba za Amana na Mikopo Inayotolewa Benki za Biashara**




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 4.7b: Riba katika Masoko ya Fedha**




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## 4.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25, utekelezaji wa bajeti ya Serikali ulikuwa wa kuridhisha. Kwa upande wa Tanzania bara, mapato ya ndani yalifikia lengo, yakichangiwa zaidi na makusanyo ya kodi (Jedwali 4.3). Mwenendo huu ulitokana na kuimarika kwa shughuli za uchumi, pamoja na juhudi za Serikali kuongeza usimamizi na ukusanyaji wa kodi. Matumizi ya Serikali yalifanyika kuendana na mapato, na yalifikia asilimia 92.1 ya makadirio.

Vilevile, utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa upande wa Zanzibar ulikuwa wa kiwango cha juu katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25. Mapato ya Serikali yanayojumuisha mapato ya ndani na misaada toka nje, yalikuwa shilingi bilioni 933.4, yakivuka lengo kwa asilimia 4.8. Mapato ya ndani yalikuwa shillingi bilioni 853.8, yakivuka lengo, wakati misaada ilivuka makadirio kwa kiwango kikubwa. Mapato ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 752.8, yakivuka lengo kwa asilimia 3.6, huku mapato yasiyo ya kodi yakiwa shilingi bilioni 101, sawa na asilimia 82.7 ya lengo (Kielelezo 4.8a). Aidha, ukusanyaji wa mapato ulikuwa wa kuridhisha katika makundi yote ya kodi kutokana na maboresho yaliyofanyika katika usimamizi na ukusanyaji kodi na pamoja na utayari wa walipakodi katika kulipa kodi kwa hiyari. Matumizi ya serikali yalikuwa shillingi bilioni 1,381, ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa asilimia 54 (Kielelezo 4.8b).

## Jedwali 4.3: Muhtasari wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Tanzania Bara


*Shilingi bilioni*

| | Jul 23 - Des 23 | | Jul 24 - Des 24 | |
|---|---|---|---|---|
| | Halisi | Makadirio | Halisi | Halisi/Makadirio (%) |
| Mapato | 14,755.7 | 16,658.3 | 16,717.6 | 100.4 |
| Matumizi | 18,152.1 | 21,087.7 | 19,428.2 | 92.1 |
| Matumizi ya kawaida | 10,293.8 | 13,376.5 | 13,019.0 | 97.3 |
| Matumizi ya maendeleo | 7,858.2 | 7,711.1 | 6,409.2 | 83.1 |

*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 4.8a: Mapato ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar


*Shilingi billioni*




*Chanzo*: Wizara ya Fedha na Mipango, Zanzibar

**Kielelezo 4.8b: Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar**

*Shilingi bilioni*




*Chanzo*: Wizara ya Fedha na Mipango, Zanzibar

## 4.6 Deni la Taifa

Deni la Serikali linalojumuisha deni la ndani na la nje lilifikia dola za Marekani bilioni 39,121.9 mwishoni mwa Desemba 2024, ambapo deni la nje lilikuwa asilimia 65.2 (Jedwali 4.4a). Kiasi kikubwa cha deni la nje kilikuwa ni mikopo nafuu kutoka mashirika ya kimataifa, ikifuatiwa na mikopo ya kibiashara. Sehemu kubwa ya mikopo hii ilitumika katika sekta za usafirishaji na mawasiliano (Jedwali 4.4b na 4.4c). Deni la ndani la Serikali lilifikia shilingi bilioni 32,649.3, ambapo kiasi kikubwa kilikuwa ni dhamana za Serikali za muda mrefu (Jedwali 4.4d). Deni la ndani la Zanzibar lilikuwa shilingi bilioni 1,247.4, ambapo kiasi kikubwa kilikuwa dhamana za Serikali na mikopo kutoka benki za biashara.

## Jedwali 4.4a: Deni la Taifa

*Dola milioni*

| | Des-23 | Jun-24 | Des-24p |
|---|---|---|---|
| Deni la Serikali kuu | 35,574.0 | 36,732.4 | 39,121.9 |
| Deni la nje | 23,422.0 | 24,569.4 | 25,488.3 |
| % ya deni la Serikali | 65.8 | 66.9 | 65.2 |
| Deni la ndani | 12,152.0 | 12,163.0 | 13,633.7 |
| Deni la nje la sekta binafsi | 6,954.5 | 7,377.7 | 7,436.4 |
| Deni la nje la mashirika ya umma | 5.0 | 3.8 | 3.8 |
| Jumla ya deni la nje | 30,381.5 | 31,950.9 | 32,928.4 |
| Jumla ya deni la Taifa | 42,533.5 | 44,113.8 | 46,562.1 |

*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
*Ufafanuzi:* *Inajumuisha mkopo wa kawaida wa benki ya biashara*; na p inamaanisha takwimu za awali*

## Jedwali 4.4b: Wadai wa Deni la Nje

*Dola milioni*

| | Des-23 | | Jun-24 | | Des-24p | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Aina ya wakopeshaji | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia |
| Mashirika ya kimataifa | 16,097.5 | 53.0 | 17,148.6 | 53.7 | 18,229.0 | 55.4 |
| Deni ambalo halijalipwa | 16,006.2 | 52.7 | 17,052.9 | 53.4 | 18,116.6 | 55.0 |
| Malimbikizo ya riba | 91.3 | 0.3 | 95.6 | 0.3 | 112.4 | 0.3 |
| Nchi wahisani | 1,432.7 | 4.7 | 1,360.2 | 4.3 | 1,369.1 | 4.2 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,180.8 | 3.9 | 1,108.4 | 3.5 | 1,117.4 | 3.4 |
| Malimbikizo ya riba | 251.9 | 0.8 | 251.9 | 0.8 | 251.7 | 0.8 |
| Kibiashara | 11,168.0 | 36.8 | 11,742.1 | 36.8 | 11,706.6 | 35.6 |
| Deni ambalo halijalipwa | 10,598.3 | 34.9 | 10,944.2 | 34.3 | 10,865.2 | 33.0 |
| Malimbikizo ya riba | 569.7 | 1.9 | 797.9 | 2.5 | 841.4 | 2.6 |
| Mkopo wa kuuza nje | 1,683.3 | 5.5 | 1,700.0 | 5.3 | 1,623.8 | 4.9 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,311.1 | 4.3 | 1,310.5 | 4.1 | 1,268.9 | 3.9 |
| Malimbikizo ya riba | 372.3 | 1.2 | 389.5 | 1.2 | 354.9 | 1.1 |
| Deni la nje | 30,381.5 | 100.0 | 31,950.9 | 100.0 | 32,928.4 | 100.0 |

*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
*Ufafanuzi:* *Inajumuisha mkopo wa kawaida wa benki ya biashara*; na p inamaanisha takwimu za awali*

## Jedwali 4.4c: Matumizi ya Mikopo ya Nje Iliyopokelewa

*Dola milioni*

| | Des-23 | | Jun-24 | | Des-24$^p$ | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Shughuli ya kiuchumi | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia |
| Urari wa malipo na msaada wa kibajeti | 4,876.5 | 16.8 | 5,358.1 | 17.6 | 6,090.6 | 19.4 |
| Usafirishaji na mawasiliano | 6,269.4 | 21.5 | 6,470.5 | 21.3 | 6,664.6 | 21.2 |
| Kilimo | 1,521.8 | 5.2 | 1,561.1 | 5.1 | 1,542.6 | 4.9 |
| Nishati na madini | 4,419.2 | 15.2 | 4,625.1 | 15.2 | 4,568.4 | 14.6 |
| Viwanda | 1,198.5 | 4.1 | 1,224.0 | 4.0 | 1,198.9 | 3.8 |
| Huduma za jamii na elimu | 5,653.5 | 19.4 | 6,181.3 | 20.3 | 6,363.9 | 20.3 |
| Fedha na bima | 1,190.8 | 4.1 | 1,197.2 | 3.9 | 1,301.2 | 4.1 |
| Utalii | 487.9 | 1.7 | 508.4 | 1.7 | 504.1 | 1.6 |
| Mali isiyohamishika na ujenzi | 1,593.8 | 5.5 | 1,521.5 | 5.0 | 1,475.0 | 4.7 |
| Mengineyo | 1,885.0 | 6.5 | 1,768.8 | 5.8 | 1,658.8 | 5.3 |
| Jumla | 29,096.5 | 100.0 | 30,416.1 | 100.0 | 31,368.0 | 100.0 |

*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
*Ufafanuzi:* *Inajumuisha mkopo wa kawaida wa benki ya biashara; *na p inamaanisha takwimu za awali*

## Jedwali 4.4d: Deni la Ndani

*Shilingi milioni*

| Nyenzo | Des-23 | | Jun-24 | | Des-24$^p$ | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia |
| Dhamana za Serikali | 26,072.4 | 85.0 | 27,266.8 | 85.3 | 28,664.3 | 87.8 |
| Dhamana za Serikali za muda mfupi | 2,730.6 | 8.9 | 2,328.7 | 7.3 | 2,108.0 | 6.5 |
| Hisa za serikali | 187.1 | 0.6 | 187.1 | 0.6 | 187.1 | 0.6 |
| Dhamana za Serikali za muda mrefu | 23,154.6 | 75.5 | 24,751.0 | 77.5 | 26,369.1 | 80.8 |
| Vyeti vya ushuru | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 |
| Deni lisilo na dhamana | 4,606.4 | 15.0 | 4,684.5 | 14.7 | 3,985.0 | 12.2 |
| Madeni mengine* | 18.4 | 0.1 | 18.4 | 0.1 | 18.4 | 0.1 |
| Bakaa hasi | 4,588.0 | 15.0 | 4,666.1 | 14.6 | 3,966.6 | 12.1 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 30,678.9 | 100.0 | 31,951.2 | 100.0 | 32,649.3 | 100.0 |

*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
*Ufafanuzi:* *Inajumuisha mkopo wa kawaida wa benki ya biashara; *na p inamaanisha takwimu za awali*

Tathmini ya uhimilivu wa deni la taifa iliyofanyika Oktoba 2024, imeonesha kuwa deni la Serikali limeendelea kuwa himilivu. Uwiano wa thamani ya sasa (*Present Value*) ya deni la Serikali kwa pato la taifa ilikuwa asilimia 41.1, ambayo ni chini ya ukomo wa uhimilivu wa deni ulioainishwa katika mwongozo wa uhimilivu wa deni wa Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki ya Dunia wa asilimia 55 na kigezo cha mtangamano wa kiuchumi kwa nchi za Afrika Mashariki cha ukomo wa asilimia 50 ya Pato la Taifa. Vilevile deni hili lilikuwa chini ya kigezo cha mtangamano wa kiuchumi kwa nchi za SADC cha ukomo wa asilimia 60 (Jedwali 4.5).

**Jedwali 4.5: Matokeo ya Upimaji wa Uhimilivu wa Deni la Taifa kwa Mwaka 2024.**

| | Ukomo | 2023/24* | 2024/25 | 2025/26 | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2029/30 | 2034/35 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uhimilivu wa deni la Serikali | | | | | | | | | |
| Thamani ya sasa (PV) ya uwiano wa deni kwa Pato la Taifa | 55 | 41.1 | 40.3 | 39.5 | 38.1 | 36.8 | 36.5 | 36.4 | 35.9 |
| Thamani ya sasa (PV) ya uwiano wa deni kwa mapato na misaada | N/A | 267.6 | 251.1 | 241.3 | 232.1 | 224.4 | 222.3 | 221.7 | 219 |
| Uwiano wa ulipaji wa deni kwa mapato na misaada | N/A | 35.4 | 50.9 | 40.8 | 37.1 | 35.9 | 36.1 | 39.9 | 37 |
| Uhimilivu wa deni la nje | | | | | | | | | |
| Thamani ya Sasa (PV) ya uwiano wa deni kwa Pato la Taifa | 40 | 23.6 | 24.1 | 24 | 23 | 21.4 | 20.3 | 19.6 | 16.6 |
| Thamani ya Sasa (PV) yauwiano wa deni kwa mauzo ya nje | 180 | 127.5 | 123.8 | 124.5 | 119.5 | 111.9 | 106.4 | 100.3 | 85.2 |
| Uwiano wa ulipaji wa deni kwa mauzo ya nje | 15 | 11.7 | 13.9 | 12.8 | 12.3 | 12.8 | 12.6 | 12.4 | 9 |
| Uwiano wa ulipaji wa deni kwa mapato | 18 | 14.5 | 17.2 | 15.5 | 14.8 | 15.2 | 14.8 | 15 | 10.9 |

*Chanzo:* Wizara ya Fedha
*Ufafanuzi:* (*) inamanisha takwimu halisi mpaka kufikia mwisho wa Juni 2024, N/A inamaanisha haihusiki

## 4. 7 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Sekta ya nje iliimarika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25, sanjari na mwenendo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini[6]. Urari wa malipo ya kawaida (*current account*) unakadiriwa kuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 785.3, ikiwa ni takriban nusu ya nakisi iliyorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24 kutokana na kuongezeka kwa mapato ya utalii, mauzo ya dhahabu, na bidhaa asilia (Jedwali 4.6). Kwa mwaka 2024, urari wa malipo ya kawaida ulikuwa dola za Marekani milioni 2,113.5 (sawa na asilimia 2.7 ya Pato la Taifa), ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,958.3 mwaka 2023 (sawa na asilimia 3.7 ya pato la Taifa) (Kielelezo 4.9).

6 Takwimu zote za mwaka 2024 bado ni makadirio ya awali.

## Jedwali 4.6: Urari wa Malipo ya Kawaida


*Dola millioni*

| | Mwaka | | | Julai - Desemba | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2022 | 2023 | 2024p | 2023 | 2024p |
| Urari wa bidhaa | -6,984.9 | -6,032.3 | -5,174.9 | -2,976.5 | -2,235.5 |
| Zilizouzwa nje* | 7,223.8 | 7,696.6 | 9,144.8 | 4,325.9 | 5,601.2 |
| Zilizonunuliwa nje | -14,208.7 | -13,728.9 | -14,319.7 | -7,302.3 | -7,836.7 |
| Urari wa huduma | 2,296.6 | 3,953.9 | 4,478.1 | 2,335.2 | 2,260.5 |
| Mapato | 4,762.0 | 6,283.7 | 6,948.2 | 3,516.9 | 3,670.7 |
| Malipo | -2,465.4 | -2,329.8 | -2,470.1 | -1,181.7 | -1,410.2 |
| Urari wa Bidhaa na Huduma | -4,688.3 | -2,078.4 | -696.8 | -641.3 | 25.0 |
| Bidhaa na Huduma zilizouzwa nje | 11,985.8 | 13,980.3 | 16,093.1 | 7,842.8 | 9,272.0 |
| Bidhaa na Huduma zilizonunuliwa kutoka nje | -16,674.1 | -16,058.7 | -16,789.8 | -8,484.1 | -9,246.9 |
| Urari wa mapato ya vitega uchumi | -1,393.2 | -1,536.0 | -1,893.4 | -821.2 | -1,049.4 |
| Yaliyoingia | 183.9 | 189.8 | 218.3 | 95.7 | 117.1 |
| Yaliyotoka | -1,577.1 | -1,725.8 | -2,111.7 | -917.0 | -1,166.5 |
| Urari wa uhamisho mali ya kawaida | 599.3 | 656.1 | 476.6 | 321.2 | 239.0 |
| Iliyoingia | 716.5 | 801.4 | 677.6 | 410.4 | 339.9 |
| ambapo Serikalini | 76.4 | 109.7 | 19.9 | 52.3 | 0.0 |
| Iliyoingia | -117.2 | -145.2 | -201.0 | -89.2 | -100.9 |
| Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali | -5,482.2 | -2,958.3 | -2,113.5 | -1,141.3 | -785.3 |

*Chanzo:* Mamlaka ya Mapato Tanzania Benki Kuu ya Tanzania
*Ufafanuzi:* p inamaanisha takwimu za awali

## Kielelezo 4.9: Urari wa Malipo ya Kawaida

*Dola millioni*




*Chanzo*: Benki Kuu ya Tanzania

Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 9,272 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 7,842.8 zilizorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Mapato ya utalii, mauzo ya dhahabu na bidhaa asilia hususan korosho na tumbaku zikichangia kwa kiwango kikubwa mwenendo huu (Jedwali 4.7). Aidha, ongezeko la thamani ya mauzo ya korosho na tumbaku lilitokana na mwenendo wa bei na kiasi cha mauzo. Kwa mwaka 2024, mauzo ya bidhaa na huduma pia yaliongezeka hadi dola za Marekani milioni 16,093.1, kutoka dola za Marekani milioni 13,980.3 mwaka uliotangulia. Mauzo haya yanakadiriwa kufikia asilimia 20 ya Pato la Taifa (GDP), ikilinganishwa na asilimia 18 ya Pato la Taifa kwa mwaka uliopita.

### Jedwali 4.7: Mauzo ya Bidhaa na Huduma Nje ya Nchi

*Dola millioni*

| | Mwaka | | | Julai - Desemba | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2022 | 2023 | 2024p | 2023 | 2024p |
| Bidhaa asilia | 766.5 | 953.3 | 1,372.2 | 717.2 | 1,023.1 |
| Bidhaa zisizo asilia | 6,457.3 | 6,743.2 | 7,772.6 | 3,608.7 | 4,541.9 |
| ambapo Dhahabu | 2,835.1 | 3,058.9 | 3,369.7 | 1,636.5 | 1,884.4 |
| Bidhaa za viwandani | 1,419.2 | 1,363.3 | 1,378.8 | 697.0 | 746.9 |
| Mazao ya mboga na maua | 289.6 | 417.2 | 569.3 | 304.1 | 458.1 |
| Mapato ya huduma | 4,762.0 | 6,283.7 | 6,948.2 | 3,516.9 | 3,707.0 |
| ambapo Utalii | 2,527.8 | 3,373.8 | 3,656.7 | 1,957.0 | 1,971.2 |
| Usafirishaji | 1,872.0 | 2,423.8 | 2,702.0 | 1,301.0 | 1,404.9 |
| Mauzo ya bidhaa na huduma | 11,985.8 | 13,980.3 | 16,093.1 | 7,842.8 | 9,272.0 |

*Chanzo*: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
*Ufafanuzi:* p inamaanisha takwimu za awali

Uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi uliongezeka kwa kasi ndogo katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25 na kufikia dola za Marekani milioni 9,246.9 ukilinganishwa na dola za Marekani milioni 8,484.1 katika kipindi kama hicho mwaka uliopita (Jedwali 4.8). Aidha, thamani ya uagizaji wa bidhaa za petroli ilipungua kwa asilimia 11.2 hadi dola za Marekani milioni 1,384.6, kutokana na kushuka kwa bei katika soko la dunia. Uagizaji wa mbolea uliongezeka hadi dola za Marekani milioni 238.1 kutoka dola milioni 207.7, ukiakisi ongezeko la matumizi katika shughuli za kilimo. Katika mwaka 2024, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa toka nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 16,789.8, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 16,058.7 mwaka uliopita. Kiwango kikubwa cha bidhaa zilizoagizwa kilikuwa ni bidhaa za petroli, vyombo vya usafirishaji viwandani, chuma pamoja na bidhaa za plastiki.

## Jedwali 4.8: Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje ya Nchi

*Dola milioni*

| | Mwaka | | | Julai - Desemba | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2022 | 2023 | 2024$^p$ | 2023 | 2024$^p$ |
| Bidhaa za kukuza mtaji | 2,594.0 | 2,893.4 | 3,042.9 | 1,489.2 | 1,750.8 |
| Mashine na mitambo | 1,128.9 | 1,242.7 | 1,057.6 | 577.3 | 548.2 |
| Vifaa vya usafiri wa viwandani | 823.2 | 937.2 | 1,198.9 | 493.4 | 749.6 |
| Bidhaa za kati | 10,231.0 | 9,389.1 | 9,879.4 | 5,074.0 | 5,336.8 |
| Malighafi za viwanda | 4,780.1 | 4,307.1 | 4,643.0 | 2,356.9 | 2,582.0 |
| Mafuta na vilainishi | 3,482.9 | 2,915.7 | 2,862.6 | 1,655.9 | 1,477.1 |
| ambapo Bidhaa za petroli zilizochujwa | 3,314.8 | 2,725.8 | 2,627.8 | 1,559.0 | 1,384.6 |
| Vifaa | 987.5 | 998.6 | 1,096.4 | 499.5 | 641.7 |
| Chakula na vinywaji kwa matumizi ya viwandani | 717.9 | 828.8 | 901.6 | 393.7 | 415.6 |
| ambapo Ngano | 302.4 | 418.8 | 324.3 | 172.7 | 154.8 |
| Magari binafsi | 257.5 | 338.1 | 373.8 | 167.7 | 219.0 |
| Bidhaa za matumizi ya kawaida | 1,381.5 | 1,444.2 | 1,395.2 | 738.0 | 748.0 |
| Chakula na vinywaji kwa matumizi ya kawaida | 182.0 | 240.1 | 178.7 | 84.4 | 102.4 |
| Vifaa vya usafiri wa kawaida | 159.5 | 141.7 | 163.9 | 81.2 | 87.8 |
| Bidhaa nyingine za matumizi ya kawaida | 1,040.1 | 1,062.4 | 1,052.6 | 572.4 | 557.8 |
| Malipo ya huduma | 2,465.4 | 2,329.8 | 2,470.1 | 1,181.7 | 1,410.2 |
| o/w Usafirishaji | 1,378.4 | 1,309.7 | 1,325.0 | 664.7 | 745.9 |
| Bidhaa na huduma | 16,674.1 | 16,058.7 | 16,789.8 | 8,484.1 | 9,246.9 |

*Chanzo*: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
*Ufafanuzi:* p inamaanisha takwimu za awali

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25, urari wa malipo ya kawaida kwa upande wa Zanzibar ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 321.5, ikiongezeka kutoka ziada ya dola za Marekani milioni 219.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Mwenendo huu ulitokana na ongezeko la mapato yatokanayo na mauzo ya huduma ambayo yaliongezeka kwa asilimia 17.5 kufikia dola za Marekani milioni 610.7. Aidha, mapato yatakanayo na huduma yalichangiwa zaidi na shughuli za utalii. Urari wa malipo kwa mwaka 2024 ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 530.8 ukilinganishwa na dola za Marekani milioni 350.6 kwa mwaka uliopita (Jedwali 4.9).

Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 635.5, kutoka dola milioni 540.6 katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia, yakichangiwa kwa kiwango kikubwa na utalii na bidhaa za viwandani (Kilelezo 4.10a). Katika mwaka 2024, mauzo nje ya nchi yalifikia dola za Marekani milioni 1,101.4 kutoka dola za Marekani milioni 956.5 mwaka 2023. Uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi ulikuwa dola za Marekani milioni 325.7, takriban sawa na kiwango kilichorekodiwa mwaka 2023/24 (Kilelezo 4.10b). Katika mwaka 2024 uagizaji wa bidhaa toka nje ya nchi ulikuwa dola za Marekani milioni 591.1, kutoka dola za Marekani milioni 618 kwa mwaka uliotangulia.

## Jedwali 4.9: Urari wa Malipo ya Kawaida kwa Zanzibar


*Dola milioni*

| | Mwaka | | | Jul - Des | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2022 | 2023 | 2024p | 2022 | 2023 | 2024p |
| Urari wa bidhaa (halisi) | -390.3 | -466.7 | -439.4 | -207.9 | -239.7 | -247.5 |
| Zilizouzwa nje | 76.5 | 50.0 | 54.9 | 49.8 | 34.5 | 24.8 |
| Zilizonunuliwa kutoka nje | -466.9 | -516.7 | -494.3 | -257.6 | -274.3 | -272.3 |
| Urari wa huduma (halisi) | 756.0 | 805.3 | 949.8 | 482.8 | 452.4 | 557.4 |
| Mapato | 844.9 | 906.6 | 1,046.5 | 531.9 | 506.1 | 610.7 |
| Malipo | -88.9 | -101.3 | -96.8 | -49.1 | -53.7 | -53.3 |
| Urari wa bidhaa na huduma (halisi) | 365.7 | 338.6 | 510.3 | 274.9 | 212.7 | 309.8 |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 921.4 | 956.5 | 1,101.4 | 581.6 | 540.6 | 635.5 |
| Bishaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | -555.8 | -618.0 | -591.1 | -306.7 | -328.0 | -325.7 |
| Urari wa mapato ya msingi (halisi) | 4.3 | 10.6 | 17.9 | 4.7 | 5.8 | 10.2 |
| Yaliyoingia | 7.3 | 15.2 | 26.1 | 6.4 | 8.4 | 14.9 |
| Yaliyotoka | -3.0 | -4.6 | -8.2 | -1.6 | -2.6 | -4.7 |
| Urari wa Uhamishaji Mali (halisi) | 1.1 | 1.4 | 2.5 | 0.5 | 0.8 | 1.4 |
| Iliyoingia | 2.3 | 2.4 | 4.3 | 0.9 | 1.4 | 2.5 |
| Iliyotoka | -1.2 | -1.0 | -1.8 | -0.4 | -0.6 | -1.0 |
| Urari wa Bidhaa, huduma na uhamishaji mali | 371.1 | 350.6 | 530.8 | 280.2 | 219.2 | 321.5 |

*Chanzo*: Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania
*Ufafanuzi:* p inamaanisha takwimu za awali

## Kielelezo 4.10a: Mauzo ya Bidhaa na Huduma Nje ya Nchi kwa Zanzibar


*Dola millioni*




*Chanzo:* Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 4.10b: Uagizaji wa Bidhaa Kutoka Nje kwa Zanzibar**

*Dola millioni*




*Chanzo:* Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania


## 4. 8. Ukwasi wa Fedha za Kigeni na Viwango vya Kubadilisha Fedha za Kigeni

Katika robo ya kwanza ya mwaka 2024/25 uchumi ulikabiliwa na changamoto ya kupungua kwa ukwasi wa fedha za kigeni japo uliongezeka katika robo ya pili ya mwaka. Ongezeko hili lilitokana na kuimarika kwa mazingira ya kiuchumi duniani kufuatia kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia hususan, mafuta, na benki kuu katika nchi zilizoendelea kuanza kupunguza riba za sera ya fedha. Kupungua kwa riba za sera za fedha, kulipelekea kuimarika kwa mazingira ya upatikanaji wa fedha katika masoko ya kimataifa na kupungua kwa kasi ya kuhamisha mitaji kuelekea nchi zilizoendelea. Mwenendo huu pia ulichangiwa na kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni kutoka kwenye shughuli za utalii na mauzo ya madini, korosho, tumbaku na kahawa nje ya nchi. Vilevile, utekelezaji wa sera ya fedha uliofanywa

na Benki Kuu kwa lengo la kukabiliana na mfumuko wa bei ambao ungeweza kutokana na kupungua kwa thamani ya shilingi, ulichangia kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni yasiyo ya lazima.


Katika robo ya kwanza ya mwaka 2024/25, thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani ilishuka kutokana na kupungua kwa ukwasi wa dola za Marekani nchini. Hata hivyo, hali hii iliimarika kwa kiwango kikubwa mwishoni mwa robo ya pili (Kielelezo 4.11a). Kwa muktadha huu, shilingi iliimarika kwa asilimia 3.78 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25 ulinganisha na kushuka kwa thamani kwa asilimia 7.78 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Aidha, shilingi iliimarika kwa kiwango kikubwa katika wiki mbili za kwanza za mwezi Desemba 2024. Kufuatia mwenendo huu, matumizi ya fedha za kigeni katika kufanya miamala na upangaji wa bei za bidhaa na huduma nchini yalipungua kwa kiwango kikubwa, na soko lisilo rasmi la fedha za kigeni lilitoweka. Aidha, kiwango cha ubadilishaji fedha kinachozingatia uwiano wa biashara baina ya Tanzania na washirika wake wa kibiashara (NEER) na kiwango halisi ambacho huzingatia tofauti ya viwango vya mfumuko wa bei baina ya nchi hizi (REER) kiliimarika (Kielelezo 4.11b). Hata hivyo pamoja na kuimarika kwa thamani ya shilingi, mauzo ya bidhaa nje ya nchi yaliendelea kuwa na ushindani kwa kuwa kiwango hiki, kilikuwa juu ya mwenendo wake wa muda mrefu.

## Kielelezo 4.11a: Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji wa Fedha




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania


## Kielelezo 4.11b: Kiwango Halisi cha Ubadilishaji wa Fedha




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

Akiba ya fedha za kigeni ilikuwa ya kutosha katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Desemba 2024, akiba hii ilikuwa dola za Marekani milioni 5,546.1[7], kutoka dola za Marekani milioni 5,345.5 mwezi Juni 2024. Kiasi hiki kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa muda wa miezi 4.5, juu ya malengo ya nchi ya angalau miezi 4 ya uagizaji bidhaa na huduma nje ya nchi[8], na sawia na kiwango cha mtangamano wa kiuchumi kwa nchi za Afrika Mashariki (EAC) (Kielelezo 4.12a and 4.12b).

**Kielelezo 4.12a: Akiba ya Fedha za Kigeni**





*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

7 Kwa mujibu wa takwimu za awali

8 Miezi ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi, huondoa baadhi ya bidhaa zinazoagizwa kwa ajili ya uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja (*Foreign Direct Investment*)

**Kielelezo 4.12b: Miezi ya Uagizaji wa Bidhaa na Huduma**




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## 4.9 Mwenendo wa Sekta ya Fedha

Kufuatia utulivu wa uchumi, sekta ya fedha iliendelea kuwa thabiti, ikiwa na viwango vya chini vya vihatarishi. Sekta ya kibenki ambayo huchukua sehemu kubwa ya sekta ya fedha iliendelea kuwa na ukwasi na mtaji wa kutosha, na kutengeneza faida. Rasilimali za benki ziliongezeka sambamba na amana zikichochewa na ongezeko la huduma za uwakala wa mabenki, pamoja na ongezeko la matumizi ya mifumo ya kidijitali katika utoaji wa huduma za kibenki. Kwa muktadha huu, ukwasi katika mfumo wa kibenki ulikuwa wa kutosha, ambapo uwiano wa rasilimali zinazoweza kubadilishwa kuwa fedha ndani ya muda mfupi (*liquid assets*) kwa amana za muda mfupi ulikuwa juu ya kiwango kinachokubalika cha asilimia 20. Ubora wa rasilimali uliendelea kuimarika ambapo mikopo chechefu ilipungua hadi asilimia 3.3 Desemba 2024 kutoka asilimia 4.1 Juni 2024. Kiwango hiki kilikuwa chini ya ukomo unaovumilika na Benki Kuu wa asilimia 5, na unategemea kuendelea kupungua kadri benki zinavyoendelea kutekeleza mikakati ya kuongeza ubora wa rasilimali zao.

Aidha, Benki Kuu kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kuchukua hatua kadhaa kwa lengo la kuimarisha sekta ya fedha. Hatua hizi ni pamoja na kufanya maboresho ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha kwa kuzitaka benki za biashara kufuatilia mwenendo wa vigezo vya utoshelevu wa mitaji ikiwa ni moja kati ya hatua za kuanza kutumia vigezo vya usimamizi wa taasisi za fedha vya *Basel II na III* vinavyozingatia vihatarishi (ii) kutoa kanuni mpya kuhusu utoshelevu wa mitaji, usimamizi wa ukwasi ili kuchukua hatua sahihi zenye lengo la kufanya marekebisho kwa wakati, na (iii) kukusanya takwimu papo kwa papo kutoka benki  na taasisi za fedha ili kuboresha usimamizi wa sekta hii na hivyo kuiwezesha Benki kuu kuchukua hatua stahiki kwa wakati. Maboresho haya pia yanalenga kuwezesha wananchi kuongeza matumizi ya huduma mbalimbali za kifedha.


## 4.10 Mifumo ya Malipo

Mifumo ya malipo iliendelea kufanya kazi kwa ufanisi huku Benki ikiendelea kuiboresha kwa lengo la kurahisisha huduma na upatikanaji wake. Vilevile, Benki ilichukua hatua mbalimbali kwa lengo la kupunguza matumizi ya fedha taslimu na kuhamasisha malipo kwa njia za kidijitali. Kwa muktadha huu, mifumo ya malipo ilifanikisha kufanyika kwa miamala ya kifedha saa 24 kila siku kuendana na ajenda ya Benki ya kupunguza matumizi ya fedha taslimu na hivyo kuongeza matumizi ya malipo kidijitali. Hatua hizi ni pamoja na kutoa taarifa kwa umma inayokataza wafanyabiashara na watoa huduma za kifedha kutoza ada kwenye miamala ya kadi kwenye vituo vya malipo *(Point of Sale)*, na hivyo kuweka mkazo kwenye miongozo iliyotolewa kuhusu gharama za miamala inayofanyika kupitia Mifumo ya Malipo Makubwa (TISS) na Mfumo wa kuhamisha Fedha (EFT) iliyotolewa mwezi  Aprili 2024.

Aidha Benki Kuu iliendelea na jitihada za kuwezesha mwingiliano wa mifumo ya malipo ya ndani na nje ya nchi, kwa kukamilisha zoezi la kujumuisha washiriki kwenye Mfumo wa Malipo ya Papo kwa Papo wa (TIPS), na kuunganisha mfumo huu na ule wa Malipo ya Kielektroniki wa Serikali (GePG). Kuunganishwa kwa mifumo ya GePG na TIPS kutawawezesha wananchi kulipa ankara mbalimbali za serikali kupitia mtoa huduma yeyote wa mifumo ya malipo. Katika kuhakikisha usalama na uadilifu, Benki iliendelea kufuatilia mienendo ya mifumo ya malipo na watoa huduma hususan inayoendeshwa na watu binafsi, pamoja na vihatarishi vyake kwa kutumia mbinu mbalimbali za ufuatiliaji na ukaguzi wa moja kwa moja.


Kwa upande mwingine, matumizi ya malipo kwa njia za kidijitali yaliongezeka sambamba na kupungua kwa matumizi ya hundi. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25, idadi na thamani ya miamala iliyofanyika kwa mfumo wa EFT iliongezeka kwa asilimia 6.4 na 18.8, mtawalia, ikilinganishwa na miamala iliyofanyika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Ongezeko hili linatokana na juhudi za Serikali katika kupunguza gharama, kuongeza ufanisi wa mifumo ya malipo pamoja na mikakati ya kuwalinda watumiaji. Kwa upande mwingine, idadi na thamani ya hundi zilizo katika Shilingi ya Tanzania zilipungua kwa asilimia 17.8 na 9.7, mtawalia (Kielelezo 4.13). Vivyo hivyo, idadi na thamani ya hundi zilizo katika dola za Marekani zilipungua kwa asilimia 24.78 na 16.42, mtawalia. Simu za mkononi zimeendelea kuwezesha wananchi wasiofikiwa na huduma za benki katika kupata huduma za kifedha. Idadi na thamani ya miamala ya malipo kwa njia ya simu iliongezeka kutokana na ongezeko la wafanyabiashara wanaotumia mifumo hii pamoja na uwepo wa mazingira yanayowezesha kuhamisha fedha ndani na nje ya nchi, na kufanya miamala baina ya mitandao ya simu na benki (Kielelezo 4.14).

## Kielelezo 4.13a: Miamala ya Hundi za Shilingi





Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 4.13b: Miamala ya Hundi za Dola ya Marekani





Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 4.14a: Miamala Katika Mfumo wa Malipo Madogo ya Papo kwa Papo




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 4.14b: Malipo Kupitia Simu




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## SEHEMU YA TANO

### 5.0 MATARAJIO YA HALI YA UCHUMI

### 5.1 Mwelekeo ya Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia unatarajiwa kuimarika mwaka 2025. Ripoti iliyotolewa OECD mwezi Desemba 2024 na zile ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia zilizochapishwa mwezi Januari 2025 zinakadiria ukuaji wa uchumi wa dunia kuwa kati ya asilimia 2.7 na 3.3 mwaka 2025. Matarajio haya yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa sera za fedha na hatua zinazochukuliwa na serikali mbalimbali katika kuchochea shughuli za kiuchumi, na ongezeko la matumizi ya walaji. Hata hivyo, ripoti hizo zinaonesha kuwa matarajio haya ya ukuaji yanaweza kuathiriwa na ongezeko la kutotabirika kwa sera za kiuchumi, migogoro ya kisiasa na mabadiliko ya tabia nchi.

Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kupungua katika nchi nyingi, kutokana na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia na matokeo ya utekelezaji wa sera za fedha zilizopunguza ukwasi katika kipindi kilichopita. Kwa kuzingatia haya, Shirika la IMF linatarajia mfumuko wa bei kufikia asilimia 4.2 kwa mwaka 2025 na kupungua zaidi hadi asilimia 3.5 mwaka 2026, huku mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea ukikaribia malengo mapema ukilinganisha na nchi zinazoibukia na zile zinazoendelea kiuchumi. Hata hivyo, matarajio haya ya mfumuko wa bei yanaweza kuathiriwa na migogoro ya kisiasa, athari za mabadiliko ya tabianchi, na ongezeko la bei za nishati. Benki Kuu katika nchi zilizoendelea zinatarajiwa kuendelea kupunguza riba za sera ya fedha kwa viwango tofauti kuendana na matarajio ya ukuaji wa uchumi na mfumuko wa bei. Bei za mafuta ya nishati zinatarajiwa kuwa tulivu, kati ya dola za Marekani 72-75 kwa pipa mwaka 2025,

huku bei ya dhahabu ikitarajiwa kuendelea kuwa juu, ikikaribia dola za Marekani 2,500 kwa wakia moja[9].

## 5.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Ndani

Uchumi wa Tanzania Bara unatarajiwa kuendelea kukua kwa kasi katika nusu ya pili ya mwaka 2024/25. Pato la Taifa (GDP) linatarajiwa kukua kwa takriban asilimia 6 (sawa na ukuaji wa mwaka 2025), kutokana na sababu mbalimbali kama vile hali nzuri ya hewa, upatikanaji wa pembejeo kwa wakati, na uwekezaji unaoendelea kufanyika katika miundombinu ya umwagiliaji. Sekta ya ujenzi inatarajiwa kuendelea kushamiri kufuatia uwekezaji kwenye miradi mikubwa ya miundombinu, kama vile reli ya kisasa ya umeme (SGR), barabara, madaraja, na viwanja vya ndege. Shughuli za huduma za usafirishaji pamoja na uwepo wa umeme wa uhakika, zinatarajiwa kuchangia ukuaji huu. Vilevile, utekelezaji wa sera ya fedha na bajeti unatarajiwa kuchagiza ukuaji huu. Uchumi wa Zanzibar unatarajiwa pia kuwa imara, na kukua kwa zaidi ya asilimia 6 katika nusu ya pili ya mwaka 2024/25 na kwa wastani wa asilimia 6.8 mwaka 2025, kutokana na shughuli za utalii, ujenzi na upangaji wa majengo.

Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kuwa tulivu, katika nusu ya pili ya mwaka 2024/25, na unakadiriwa kuwa wastani wa takriban asilimia 3, huku mfumuko wa bei usiojumuisha bidhaa za nishati na vyakula visivyochakatwa ukitarajiwa kufikia asilimia 3.8. Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki chini ya lengo la asilimia 5. Mwenendo huu utachangiwa na utekelezaji wa sera madhubuti ya fedha na bajeti, uwepo wa chakula cha kutosha nchini, na utulivu wa bei za bidhaa katika soko la dunia. Aidha, matarajio ya mfumuko wa bei kuongezeka ni madogo japo yanaweza kuongezeka endapo nchi za OPEC+ zitaamua kuendelea kupunguza kiwango cha uzalishaji wa mafuta.

9 Kwa mujibu wa kanzidata ya Bloomberg, Januari 2025

# SEHEMU YA SITA

## 6.0 SERA YA FEDHA KATIKA NUSU YA PILI YA MWAKA 2024/25

### 6.1 Mwelekeo wa Sera ya Fedha

Kwa kuzingatia mwenendo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini kama ilivyoinishwa katika Sehemu ya Tano, mwelekeo wa sera ya fedha katika nusu ya pili ya mwaka 2024/25, utakuwa kama ulivyokuwa katika nusu ya kwanza. Lengo la sera ya fedha ni kuhakikisha kuwa mfumuko wa bei unabakia takriban asilimia 3, huku ikiendelea kuchochea ukuaji wa uchumi, kufikia asilimia 5.7 au zaidi. Katika kufanikisha malengo haya, Kamati ya Sera ya Fedha ya Benki Kuu katika kikao chake kilichofanyika tarehe 7 Januari 2025, iliamua kuibakiza Riba ya Benki Kuu (CBR) katika kiwango cha asilimia 6, kwa robo mwaka inayoishia Machi 2025. Aidha, CBR itakayotumika katika robo inayoishia Juni 2025 itatangazwa wiki ya kwanza ya Aprili 2025.

Benki Kuu itaendelea kutumia nyenzo zake za sera ya fedha ili kuhakikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha katika uchumi. Nyenzo hizi ni pamoja na mikopo ya muda mfupi (*repurchase agreement and reverse repurchase agreement*), uuzaji wa dhamana za serikali (*liquidity papers*), kununua au kuuza fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni (IFEM), na kubadilisha kiwango cha amana za benki kinachotakiwa kuwekwa kisheria Benki Kuu (SMR). Utekelezaji wa sera ya fedha utalenga kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku 7 baina ya benki inabaki ndani ya wigo wa asilimia +/- 2 ya riba ya Benki Kuu. Utekelezaji huu pia unajielekeza kufikiwa kwa malengo ya robo mwaka ya rasilimali halisi za ndani za Benki Kuu (*net domestic assets*) na akiba halisi ya fedha za kigeni (*net international reserves*) kama yalivyoainishwa katika Programu ya *Extended Credit Facility* (ECF) chini ya shirika la IMF.

Katika kuongeza ufanisi wa sera ya fedha, Benki Kuu itaendelea kufanya maboresho mbalimbali katika soko la fedha baina ya benki. Maboresho haya ni pamoja na kufanya marejeo ya dhamana zinazotumiwa na benki za biashara wakati wa kukopa toka Benki kuu, na viwango vya riba ya mikopo ya siku moja (*lombard loans*) na nyenzo nyingine zinazotumika katika utekelezaji wa sera ya fedha. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kufanya maboresho katika sekta ya fedha ikiwemo kuweka mazingira yatakayopelekea mgawanyo sawia wa ukwasi baina ya benki za biashara, kuhakikisha uthabiti wa sekta ya fedha na huduma jumuishi za kifedha, Benki Kuu itaendelelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu mfumo wa utekelezaji wa sera ya fedha kwa kutumia riba, na umuhimu wa kutumia Shilingi ya Tanzania katika kufanya miamala ya bidhaa na huduma hapa nchini. Hatua hizi ni sehemu ya kuongeza ufanisi wa sera ya fedha katika kufikia malengo yake.

## 6.2 Sera ya Riba

Viwango vya riba vitaendelea kuamuliwa na nguvu ya soko. Kamati ya sera ya fedha itaendelea kupanga Riba ya Benki Kuu ambayo itatoa mwongozo kwa riba zinazopangwa kwenye soko la mikopo baina ya benki za biashara ambazo kwa kuzingatia nguvu ya soko. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kufanya maboresho katika sekta ya fedha ili kuunga mkono jitihada za Serkali katika kuhakisha upangaji sahihi wa viwango vya riba nchini. Katika kutekeleza haya, Benki Kuu itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya fedha ili kumlinda mtumiaji wa huduma za fedha, kutoa elimu ya fedha na huduma jumuishi za kifedha.

## 6.3 Sera ya Ubadilishaji Fedha za Kigeni na Akiba ya Fedha za Kigeni

Viwango vya ubadilishaji fedha za kigeni vitaendelea kuamuliwa na nguvu ya soko. Hii itapunguza athari zinazotokana na mtikisiko wa uchumi wa dunia kwa uchumi wetu. Benki Kuu itaendelea kushiriki katika soko la jumla la fedha za kigeni (IFEM) kwa mujibu wa Sera ya Ushiriki ya Soko la Fedha za Kigeni (*Foreign Exchange Intervention Policy 2023*), kwa lengo la kupunguza mabadiliko ya mara kwa mara ya thamani ya shilingi, kuongeza akiba ya fedha za kigeni, kufanikisha utekelezaji wa sera ya fedha na kuongeza ukwasi wa fedha za kigeni katika uchumi. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kuhakikisha uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni itakayotumika kama kinga dhidi ya mitikisiko ya kiuchumi kutoka nje ya nchi, na kuhakikisha kuwa benki za biashara zinashiriki katika soko la fedha za kigeni kwa kuzingatia miongozo iliyopo.

# VIAMBATISHO

## Jedwali 1: Tanzania Bara: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi

*Asilimia*

| | 2021 | | | | 2022 | | | | 2023[p] | | | | 2024 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Shughuli za kiuchumi | Q1 | Q2 | Q3 | Q4 | Q1 | Q2 | Q3 | Q4 | Q1 | Q2 | Q3 | Q4 | Q1 | Q2 | Q3 |
| Kilimo | 2.1 | 2.5 | 4.9 | 6.2 | 4.2 | 3.8 | 3.9 | 1.9 | 5.0 | 3.1 | 5.2 | 4.1 | 3.1 | 4.2 | 4.3 |
| Uchimbaji madini na mawe | 9.0 | 9.4 | 12.4 | 7.0 | 9.7 | 5.8 | 9.6 | 17.5 | 14.2 | 10.5 | 14.3 | 6.9 | 3.5 | 6.7 | 8.6 |
| Viwanda | 6.1 | 4.5 | 3.8 | 5.0 | 6.3 | 4.7 | 4.4 | 1.8 | 5.3 | 4.3 | 4.2 | 3.6 | 5.8 | 4.6 | 5.0 |
| Umeme | 7.0 | 11.9 | 10.0 | 11.0 | 9.4 | 9.6 | 9.7 | 2.3 | 3.6 | 6.2 | 3.3 | 2.7 | 7.6 | 11.0 | 27.8 |
| Maji | 9.0 | 8.4 | 4.5 | 4.9 | 11.9 | 9.5 | 0.1 | 2.2 | 5.1 | 3.3 | 1.8 | 0.1 | 3.1 | 3.5 | 3.7 |
| Ujenzi | 4.4 | 0.5 | 4.6 | 4.0 | 6.5 | 2.9 | 1.8 | 4.8 | 5.1 | 2.3 | 3.7 | 2.9 | 6.4 | 2.9 | 3.9 |
| Biashara na matengenezo | 2.3 | 4.2 | 1.5 | 4.9 | 7.2 | 6.7 | 1.9 | 0.6 | 2.7 | 4.1 | 4.3 | 5.8 | 5.3 | 4.3 | 4.5 |
| Malazi na huduma ya chakula | -6.5 | 10.1 | 14.3 | 11.3 | 1.5 | 13.0 | 13.2 | 8.5 | 12.3 | 7.2 | 7.4 | 6.7 | 7.2 | 5.5 | 5.8 |
| Usafirishaji na uhifadhi mizigo | 9.0 | 4.9 | -0.6 | 1.2 | 1.3 | 4.1 | 7.3 | 2.7 | 2.3 | 3.9 | 5.3 | 4.6 | 7.6 | 5.8 | 6.2 |
| Habari na mawasiliano | 8.8 | 11.8 | 8.2 | 7.6 | 5.9 | 6.4 | 10.8 | 6.8 | 3.5 | 6.2 | 11.3 | 9.7 | 13.4 | 11.3 | 12.5 |
| Fedha na bima | 1.9 | 3.2 | 4.1 | 7.8 | 9.6 | 9.7 | 8.7 | 8.9 | 10.0 | 12.5 | 13.2 | 13.2 | 17.1 | 16.1 | 18.2 |
| Utawala na ulinzi | 2.6 | 4.3 | 6.5 | 6.8 | 4.6 | 4.0 | 6.7 | 6.3 | 6.7 | 5.9 | 5.3 | 4.5 | 6.6 | 6.4 | 6.6 |
| Sughuli za kitaaluma, sayansi na ufundi | 7.8 | 7.6 | 5.8 | 6.2 | 5.0 | 5.5 | 6.8 | 5.9 | 5.3 | 4.7 | 4.1 | 8.0 | 4.5 | 4.8 | 4.2 |
| Huduma zinazohusiana na utawala | 7.4 | 7.3 | 6.0 | 7.0 | 6.0 | 5.2 | 3.6 | 3.7 | 5.5 | 5.8 | 5.6 | 2.9 | 5.2 | 5.4 | 5.7 |
| Upangishaji majengo | 4.6 | 4.6 | 4.6 | 4.1 | 4.5 | 4.4 | 4.4 | 4.4 | 4.1 | 4.2 | 4.2 | 4.6 | 4.2 | 4.3 | 4.3 |
| Elimu | 5.1 | 4.8 | 6.1 | 4.4 | 6.6 | 5.2 | 6.5 | 2.9 | 6.9 | 6.5 | 6.1 | 5.2 | 4.6 | 4.3 | 6.7 |
| Afya | 4.8 | 5.5 | 7.1 | 5.6 | 4.9 | 5.5 | 7.1 | 4.1 | 5.9 | 6.3 | 6.0 | 5.8 | 3.9 | 4.1 | 5.6 |
| Huduma nyingine za kijamii | 6.6 | 10.8 | 12.1 | 11.7 | 8.5 | 7.5 | 9.0 | 9.4 | 9.5 | 11.5 | 8.9 | 7.2 | 8.6 | 9.9 | 8.8 |
| Shughuli zote za viwandani kwa bei za msingi | 4.3 | 3.9 | 4.7 | 5.4 | 5.5 | 4.8 | 4.9 | 4.0 | 5.5 | 4.6 | 5.8 | 4.8 | 5.7 | 5.2 | 6.1 |
| Kodi katika bidhaa | 8.4 | -0.9 | 11.5 | 10.9 | 12.5 | 7.5 | -0.5 | -3.0 | -1.5 | 6.2 | 2.5 | 7.9 | 3.7 | 6.6 | 3.7 |
| Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko | 4.5 | 3.6 | 5.3 | 5.8 | 6.0 | 4.9 | 4.5 | 3.4 | 5.0 | 4.7 | 5.6 | 5.0 | 5.6 | 5.3 | 5.9 |

*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

# Jedwali 2: Zanzibar: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi

*Asilimia*

| | 2021 | | | | 2022 | | | | 2023 | | | | 2024 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Shughuli za kiuchumi | Q1 | Q2 | Q3 | Q4 | Q1 | Q2 | Q3 | Q4 | Q1 | Q2 | Q3 | Q4 | Q1 | Q2 | Q3 |
| Kilimo cha mazao | 6.7 | 10.2 | 5.5 | 0.7 | -9.5 | -8.6 | -3.2 | 20.5 | 10.4 | 6.1 | 3.7 | 1.6 | 7.1 | 13.1 | 2.5 |
| Ufugaji | 25.5 | 8.7 | 9.4 | 83.7 | -34.4 | -9.6 | -11.1 | 11.5 | 26.4 | -5.2 | -5.0 | -28.3 | -28.7 | -20.0 | -15.0 |
| Misitu | -3.2 | 4.2 | 6.2 | 6.8 | 3.8 | 3.7 | 2.0 | 4.3 | 9.7 | 7.5 | -1.2 | 2.9 | 3.4 | 1.4 | 4.3 |
| Uvuvi | -3.5 | -5.1 | -43.7 | -4.8 | 21.7 | -5.8 | 47.5 | 93.9 | 5.5 | -0.3 | 15.7 | -17.3 | 7.2 | 29.2 | 22.8 |
| Uchimbaji madini na mawe | -26.4 | 5.2 | 22.6 | 18.0 | 19.1 | 15.0 | 1.9 | 18.7 | 37.4 | 41.4 | 0.6 | -25.3 | 1.5 | 20.9 | 8.9 |
| Viwanda | 10.6 | 8.3 | 3.7 | -3.5 | 9.2 | 3.1 | 0.5 | 14.3 | 5.9 | 4.5 | 2.2 | 7.1 | 5.1 | 4.2 | 5.8 |
| Umeme | 4.8 | 37.8 | 20.6 | -9.6 | 11.9 | -9.6 | 20.1 | 8.0 | 0.2 | 19.6 | 12.1 | 30.3 | 7.9 | 9.4 | 0.6 |
| Huduma za maji | 10.6 | 8.7 | 10.4 | 10.7 | 5.0 | 6.5 | 1.1 | 6.6 | 4.8 | 6.8 | 3.0 | 0.4 | 4.6 | -2.0 | 11.4 |
| Ujenzi | -36.2 | -28.6 | 6.9 | 151.1 | 65.6 | 10.6 | 8.2 | -14.1 | 22.7 | 7.2 | 23.9 | -9.6 | -5.0 | 14.4 | 10.4 |
| Biashara | 1.4 | 3.0 | 26.2 | 19.6 | 3.0 | 15.7 | 1.8 | 17.5 | 33.5 | 2.0 | -8.9 | 5.8 | 1.6 | 11.4 | 11.2 |
| Malazi na huduma ya chakula | 3.0 | 90.6 | 5.0 | 10.6 | 5.6 | 25.2 | 19.8 | 15.2 | 13.6 | 16.9 | 28.5 | 4.4 | 4.5 | 13.8 | 14.9 |
| Usafirishaji na uhifadhi mizigo | 4.8 | 7.3 | 23.3 | 8.8 | -1.8 | 2.8 | -3.8 | 11.6 | 11.9 | 21.4 | 3.3 | 3.7 | 1.8 | 4.2 | -2.6 |
| Habari na mawasiliano | -4.9 | -35.2 | 2.6 | -38.3 | -40.3 | 13.1 | -11.1 | 0.0 | 32.1 | -2.5 | 11.6 | 0.4 | 1.6 | 1.5 | 5.7 |
| Fedha na bima | 22.4 | -5.1 | 32.6 | 16.4 | -0.2 | 11.5 | 4.7 | 12.7 | 92.8 | 30.4 | 0.1 | 69.0 | 7.4 | 0.3 | 6.0 |
| Upangishaji majengo | 6.9 | 6.9 | 7.0 | 6.9 | 7.0 | 7.1 | 7.1 | 7.1 | 7.8 | 8.1 | 4.6 | 8.4 | 7.8 | 7.6 | 11.2 |
| Sughuli za kitaaluma, sayansi na ufundi | 7.9 | -60.3 | 8.5 | 28.7 | 29.0 | 80.6 | 4.3 | 0.0 | -27.8 | 41.3 | 14.2 | 0.0 | 4.9 | 19.5 | 2.0 |
| Huduma zinazohusiana na utawala | -16.8 | -47.1 | 26.7 | 18.7 | 14.0 | 45.0 | 0.5 | 37.9 | 4.7 | 30.6 | 39.4 | 0.0 | 2.5 | 8.4 | 6.8 |
| Utawala na ulinzi | 26.2 | 23.2 | 22.8 | -19.1 | 4.5 | -16.7 | 0.0 | 5.1 | 1.5 | 3.3 | 4.2 | 12.2 | 3.2 | 1.7 | 2.9 |
| Elimu | -5.1 | -7.8 | -6.3 | -9.9 | 19.9 | 11.6 | 7.6 | 0.0 | 7.8 | 8.0 | 6.7 | 0.0 | 0.6 | 5.9 | 8.9 |
| Afya na huduma za jamii | 15.4 | 14.6 | 30.3 | 1.8 | -3.2 | 17.4 | -0.4 | 5.2 | 27.2 | -9.2 | 0.8 | 0.0 | 5.1 | 8.4 | 5.1 |
| Sanaa na burudani | 2.9 | -40.1 | 40.3 | -18.7 | 5.5 | 63.8 | 37.8 | 0.0 | 17.2 | 33.8 | -14.9 | 0.2 | 8.7 | 8.0 | 1.5 |
| Huduma nyingine za kijamii | 29.4 | -30.5 | 41.9 | -5.8 | 11.5 | 38.0 | 6.5 | -20.5 | -7.3 | 17.6 | 16.2 | 0.0 | 3.3 | 3.9 | 7.1 |
| Shughuli za kaya katika kuajiri | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 2.4 | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 0.0 | 3.2 | 2.4 | 1.6 | 0.1 | 3.2 | 3.2 | 3.2 |
| Gharama za kifedha zilizojificha (FISIM) | 42.0 | 9.5 | 53.1 | -2.0 | -18.9 | 6.0 | -21.6 | 0.0 | 76.9 | 7.2 | 9.0 | 0.0 | 7.8 | 2.4 | 8.1 |
| Shughuli zote za viwandani kwa bei za msingi | 3.7 | 6.6 | 6.4 | 15.3 | 4.3 | 3.7 | 1.5 | 10.9 | 15.5 | 7.7 | 13.7 | 2.0 | 1.7 | 7.4 | 8.0 |
| Kodi za bidhaa | -11.0 | 5.9 | 29.6 | 7.4 | 13.1 | 38.0 | -6.3 | -31.2 | 6.6 | -7.1 | -7.5 | 6.0 | 2.8 | 6.1 | 2.7 |
| Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko | 2.2 | 6.5 | 8.8 | 3.0 | 5.1 | 6.6 | 4.2 | 8.4 | 9.7 | 6.1 | 7.4 | 2.2 | 6.4 | 7.2 | 7.5 |

*Chanzo:* Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali-Zanzibar

## Jedwali 3: Takwimu za Kifedha

*Shilingi billioni*

| | Dec-22 | Mar-23 | Jun-23 | Sep-23 | Dec-23 | Mar-24 | Jun-24 | Sep-24 | Dec-24 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Rasilimali halisi za nje | 9,437.5 | 8,697.1 | 10,455.1 | 10,121.6 | 11,302.4 | 11,635.0 | 12,238.3 | 13,704.3 | 13,583.9 |
| Rasilimali halisi za ndani | 29,142.5 | 30,416.1 | 31,729.8 | 33,019.5 | 32,706.2 | 32,892.4 | 34,523.8 | 34,360.2 | 35,321.5 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 27,372.5 | 28,535.7 | 29,835.6 | 30,791.3 | 32,102.0 | 33,346.2 | 34,980.8 | 36,174.1 | 36,097.4 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi | 38,580.0 | 39,113.2 | 42,185.0 | 43,141.0 | 44,008.6 | 44,527.4 | 46,762.1 | 48,064.6 | 48,905.3 |
| Amana za fedha za kigeni kwa Shilingi | 8,201.1 | 8,617.7 | 9,591.3 | 9,715.9 | 10,000.8 | 10,397.3 | 11,496.1 | 12,427.9 | 11,765.3 |
| *Amana za fedha za kigeni (Dola milioni)* | *3,552.2* | *3,729.5* | *4,128.8* | *3,940.5* | *4,004.6* | *4,083.6* | *4,400.8* | *4,609.6* | *4,829.2* |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana | 30,378.9 | 30,495.5 | 32,593.7 | 33,425.2 | 34,007.8 | 34,130.1 | 35,266.0 | 35,636.6 | 37,140.1 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu | 18,948.2 | 18,618.7 | 20,352.4 | 20,611.2 | 20,600.2 | 20,862.9 | 21,995.8 | 21,825.4 | 22,905.8 |
| Fedha zilizopo kwenye mzunguko | 5,709.0 | 5,371.1 | 6,161.5 | 6,475.9 | 6,485.0 | 6,325.5 | 7,076.5 | 7,353.5 | 7,351.9 |
| Amana za hundi | 13,239.2 | 13,247.5 | 14,190.9 | 14,135.3 | 14,115.2 | 14,537.3 | 14,919.3 | 14,471.9 | 15,553.9 |
| Viashiria vinginevyo | | | | | | | | | |
| Fedha taslimu | 9,736.3 | 9,236.4 | 10,850.7 | 9,943.7 | 10,099.8 | 10,185.5 | 10,926.3 | 11,133.7 | 12,024.8 |
| Akiba za benki | 2,987.9 | 2,893.0 | 3,658.6 | 2,411.2 | 2,444.5 | 2,907.0 | 2,886.6 | 2,667.0 | 3,351.5 |
| Fedha zilizo nje ya Benki Kuu ya Tanzania | 6,748.3 | 6,343.4 | 7,192.0 | 7,532.5 | 7,655.3 | 7,278.5 | 8,039.7 | 8,466.7 | 8,673.3 |
| Kiwango cha ubadilishaji fedha (Shilingi ya Tanzania/Dola ya Marekani) | 2,308.7 | 2,310.7 | 2,323.0 | 2,465.6 | 2,497.4 | 2,546.1 | 2,612.2 | 2,696.1 | 2,436.3 |
| Viwango vya ukuaji wa kila mwaka (%) | | | | | | | | | |
| Fedha taslimu | 15.8 | 10.2 | 17.0 | 3.9 | 3.7 | 10.3 | 0.7 | 12.0 | 19.1 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi | 11.6 | 15.9 | 18.8 | 14.5 | 14.1 | 13.8 | 10.9 | 11.4 | 11.1 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana | 12.1 | 15.1 | 18.0 | 14.0 | 11.9 | 11.9 | 8.2 | 6.6 | 9.2 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 22.5 | 22.9 | 21.3 | 19.5 | 17.3 | 16.9 | 17.2 | 17.5 | 12.4 |

*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

# Jedwali 4: Riba za Masoko ya Fedha na Mitaji

*Asilimia*

| Aina ya riba | Dec-23 | Jan-24 | Feb-24 | Mar-24 | Apr-24 | May-24 | Jun-24 | Jul-24 | Aug-24 | Sep-24 | Oct-24 | Nov-24 | Dec-24 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Riba katika soko la fedha baina ya mabenki | | | | | | | | | | | | | |
| Siku 1 (Overnight) | 6.56 | 6.75 | 6.35 | 6.20 | 6.51 | 7.02 | 6.92 | 6.80 | 7.62 | 7.88 | 7.74 | 7.73 | 7.07 |
| Siku 2-7 | 6.89 | 7.29 | 7.20 | 7.17 | 7.04 | 7.35 | 7.40 | 7.42 | 7.83 | 8.26 | 8.17 | 8.11 | 7.38 |
| Riba ya jumla | 6.81 | 7.27 | 7.20 | 7.10 | 7.02 | 7.34 | 7.36 | 7.24 | 7.79 | 8.16 | 8.04 | 8.06 | 7.41 |
| Riba ya mikopo ya siku 1 kati ya mabenki na Benki Kuu (Lombard rate) | 9.84 | 7.50 | 7.50 | 7.50 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 |
| Riba ya mikataba ya mauziano ya dhamana za muda mfupi (Reverse REPO rate) | 6.29 | 6.29 | 5.81 | 5.74 | 6.57 | 6.57 | 6.57 | 6.57 | 7.88 | 8.00 | 8.00 | 7.72 | 7.72 |
| Riba ya dhamana za serikali | | | | | | | | | | | | | |
| Siku 182 | 9.40 | 9.30 | 8.93 | 8.61 | 8.45 | 8.22 | 6.57 | 6.57 | 7.30 | 7.30 | 8.17 | 8.30 | 8.30 |
| Siku 364 | 10.51 | 11.81 | 12.25 | 11.82 | 10.38 | 7.83 | 6.75 | 8.84 | 10.63 | 10.98 | 11.66 | 12.78 | 12.95 |
| Riba ya jumla | 10.48 | 11.76 | 12.21 | 11.65 | 10.33 | 7.86 | 6.75 | 8.81 | 10.61 | 10.85 | 11.55 | 12.68 | 12.95 |
| Riba za hati fungani za serikali | | | | | | | | | | | | | |
| Miaka miwili | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 |
| Miaka mitano | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 12.41 | 12.41 | 12.41 |
| Miaka saba | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 |
| Miaka kumi | 11.85 | 12.03 | 12.03 | 12.03 | 12.30 | 12.30 | 12.30 | 12.30 | 13.26 | 13.26 | 13.26 | 13.26 | 13.26 |
| Miaka kumi na tano | 12.75 | 12.75 | 13.66 | 13.66 | 13.66 | 15.16 | 15.16 | 15.05 | 15.05 | 15.35 | 15.76 | 15.76 | 15.76 |
| Miaka ishirini | 13.51 | 13.51 | 15.83 | 15.51 | 15.24 | 15.24 | 15.13 | 15.17 | 15.40 | 15.45 | 15.76 | 15.64 | 15.71 |
| Miaka ishirini na tano | 14.39 | 14.39 | 14.39 | 16.79 | 16.13 | 16.13 | 15.38 | 15.38 | 15.38 | 15.42 | 15.42 | 15.93 | 15.93 |
| Riba ya Benki Kuu | | 5.50 | 5.50 | 5.50 | 6.00 | 6.00 | 6.00 | 6.00 | 6.00 | 6.00 | 6.00 | 6.00 | 6.00 |

*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## Jedwali 5: Riba za Mabenki

*Asilimia*

| Aina ya riba | Dec-23 | Jan-24 | Feb-24 | Mar-24 | Apr-24 | May-24 | Jun-24 | Jul-24 | Aug-24 | Sep-24 | Oct-24 | Nov-24 | Dec-24 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A: Shilingi ya Tanzania | | | | | | | | | | | | | |
| Riba za amana | 2.60 | 2.69 | 2.54 | 2.70 | 2.79 | 2.87 | 2.86 | 2.87 | 3.02 | 2.84 | 2.85 | 2.69 | 2.84 |
| Riba za jumla za amana za | | | | | | | | | | | | | |
| muda maalum | 7.45 | 7.40 | 7.39 | 7.55 | 7.44 | 7.65 | 7.66 | 8.15 | 7.98 | 8.20 | 8.25 | 8.18 | 8.33 |
| Miezi sita | 9.14 | 9.13 | 9.07 | 9.15 | 9.12 | 9.37 | 9.25 | 9.09 | 8.91 | 9.15 | 9.30 | 9.19 | 9.30 |
| Mwaka mmoja | 8.92 | 9.15 | 9.06 | 8.94 | 8.21 | 8.97 | 9.09 | 9.01 | 8.82 | 9.12 | 10.41 | 9.63 | 9.62 |
| Riba za amana za wateja wakubwa | 9.19 | 9.56 | 9.52 | 9.59 | 9.33 | 9.72 | 9.86 | 9.96 | 10.12 | 9.88 | 10.27 | 10.14 | 10.39 |
| Riba za mikopo za Jumla | 15.44 | 15.39 | 15.44 | 15.51 | 15.42 | 15.47 | 15.30 | 15.29 | 15.26 | 15.54 | 15.67 | 15.67 | 15.71 |
| Muda mfupi (Hadi mwaka 1) | 15.94 | 15.82 | 16.10 | 16.17 | 15.93 | 15.98 | 15.57 | 15.67 | 15.50 | 15.67 | 16.06 | 15.56 | 15.74 |
| Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2) | 15.91 | 15.82 | 15.71 | 15.74 | 15.77 | 15.82 | 15.69 | 15.49 | 15.50 | 15.97 | 16.25 | 16.93 | 16.79 |
| Muda wa kati (Miaka 2 hadi 3) | 15.82 | 15.92 | 15.80 | 16.05 | 15.87 | 15.88 | 15.78 | 16.06 | 16.09 | 16.26 | 16.48 | 16.36 | 16.21 |
| Muda mrefu (Miaka 3 hadi 5) | 15.48 | 15.39 | 15.51 | 15.42 | 15.44 | 15.50 | 15.37 | 15.21 | 15.14 | 15.20 | 15.06 | 15.17 | 15.24 |
| | 13.38 | 13.44 | 13.40 | 13.46 | 13.95 | 12.69 | 12.82 | 12.78 | 12.79 | 12.92 | 12.93 | 12.77 | 12.83 |
| B: Fedha za kigeni | | | | | | | | | | | | | |
| Riba za amana | | | | | | | | | | | | | |
| Amana za akiba | 0.04 | 0.04 | 0.04 | 0.91 | 0.79 | 0.90 | 0.97 | 0.53 | 1.28 | 0.91 | 0.73 | 0.71 | 0.81 |
| Riba za jumla za amana za | | | | | | | | | | | | | |
| muda maalum | 3.67 | 3.40 | 3.73 | 3.82 | 3.77 | 3.65 | 3.91 | 3.97 | 3.73 | 3.68 | 3.85 | 3.99 | 4.20 |
| Miezi sita | 3.95 | 3.41 | 3.65 | 3.88 | 4.39 | 4.46 | 4.38 | 3.74 | 4.40 | 4.54 | 4.59 | 4.44 | 4.36 |
| Mwaka mmoja | 4.43 | 4.58 | 4.47 | 4.64 | 4.49 | 4.40 | 4.44 | 4.26 | 3.89 | 3.21 | 3.83 | 3.57 | 3.54 |
| Riba za mikopo za Jumla | 7.64 | 7.72 | 8.13 | 8.17 | 8.10 | 8.19 | 7.23 | 8.34 | 8.56 | 8.44 | 8.77 | 8.53 | 8.80 |
| Muda mfupi (Hadi mwaka 1) | 8.93 | 9.46 | 9.11 | 9.60 | 8.74 | 8.77 | 6.58 | 9.10 | 9.55 | 9.41 | 9.50 | 9.50 | 9.44 |
| Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2) | 7.04 | 6.90 | 7.71 | 7.77 | 7.94 | 7.89 | 7.10 | 7.48 | 7.69 | 6.75 | 7.60 | 7.74 | 7.78 |
| Muda wa kati (Miaka 2 hadi 3) | 8.21 | 8.14 | 8.44 | 8.35 | 8.47 | 8.27 | 7.63 | 8.31 | 8.28 | 8.70 | 8.76 | 8.02 | 9.19 |
| Muda mrefu (Miaka 3 hadi 5) | 6.53 | 6.67 | 7.09 | 6.49 | 6.94 | 6.94 | 6.56 | 7.35 | 7.41 | 7.52 | 8.23 | 8.01 | 8.23 |

*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Benki Kuu ya Tanzania, Barabara ya 16 ya Jakaya Kikwete 40184,
Sanduku la Posta 2303, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 296 3182-7 au +255 22 223 2541
Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz
Tovuti: https://www.bot.go.tz